MID WEEK JACKPOT!
TZS. 544,830,140
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Mke** afia ofisi ya mtendaji kuitikia wito mtalaka wake

UKURASA 3


ama
ALHAMISI APRILI 13, 2023 AFYA NA MAZINGIRA
Mikoa sita Kanda ya Ziwa inavyoteseka utapiamlo, yabuni opereshen
Tabianchi inavyotenganisha mume na mke Ukerewe
Wataalamu Ubungo waenda mtaani kufunza kinga marburg, kipindupindu, Uviko 19
WAZIRI UMMY NA ORODHA MANUFAA...
Nchini kunaposimama Kituo Mafunzo ya Usalama Ulinzi Mimea ndani ya EA

UKURASA 11

# Nipashe

Alhamisi Aprili 13, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581279

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US

# Wabunge wataka muswada wa sheria kudhibiti ushoga

• **Serikali** yaweka msimamo, shule yachunguzwa mapenzi jinsia moja...*Ukurasa 2*



KALOGERESI · TARIMBA · MAKAMBA

## Sakata ununuzi Tanga Cement kaa la moto, wabunge wapinga

UKURASA 2



## Serikali yatangaza ajira 21, 220 afya elimu, yahadharisha udanganyifu vyeti

UKURASA 3




Kampuni ya the Guardian Limited, Wachapishaji wa Magazeti ya the Guardian na Nipashe, inawakaribisha wadau wote wa maendeleo kutoa salaam za pongezi wakati tunaadhimisha miaka 59 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Toleo hili litachapishwa tarehe 26 Aprili, 2023 kwenye Magazeti ya Guardian na Nipashe.

The Guardian · Nipashe

Kwa mawasiliano zaidi,
Tupigie +255 677 020 701

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com



Magari yakiwa yamekwama na mengine yakivutwa na trekta katika barabara ya Malinyi-Ifakara, mkoani Morogoro juzi, kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha na kusababisha wasafiri na wasafirishaji wa bidhaa kukwama kwa siku nne. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Wabunge wataka muswada wa sheria kudhibiti ushoga

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WABUNGE wameitaka serikali kupeleka Bungeni, muswada wa sheria utakaokuwa na nguvu ya kudhibiti ushoga au mapenzi ya jinsia moja na kama haiwezekani Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA) ya Mwaka 1998, ifumuliwe.

Akichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2023/24, Mbunge wa Kinondoni (CCM), Tarimba Abbas, alisema mambo hayo yanaumiza vichwa vya watu wakati jambo hilo si la leo.

"Mwaka 1998 kulikuwapo na sheria ambayo ilitungwa inasema 'sexual offensives special provision act 1998; maana yake mambo haya yalikuwapo miaka mingi yanasumbua, yalikuwa madogo madogo na sheria ile haikuja kwa kificho.

"Ilikuja kwa uwazi kabisa ikionyesha jinsi ya kupiga vita vitendo hivi. Naomba kama haiwezekani kuleta sheria mpya hapa (Bungeni), basi ifumueni Sheria ya SOSPA ya Mwaka 1998 ili kukidhi mahitaji ya sasa," alisema.

Mbunge wa Morogoro Kusini (CCM), Innocent Kalogeresi, akichangia mjadala huo alisema: "Haya mambo ya haki za binadamu ni ya kuliondoa kusudi la Mungu katika taifa letu.

"Niwaombe sana Wabunge na Watanzania wapambane nalo kwa nguvu zote.

Haiwezekani tukaileta laana katika taifa hili ambalo Mungu ameliweka. Niombe sana viongozi wetu wa kitaifa, hili jambo walichukulie 'serious' (makini) na ikiwezekana pawapo na kipindi maalum cha kutubu ili kuondoa dhambi hii katika taifa hili."

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Salome Makamba, alisema kwa kuwa mkoa wa Shinyanga kitakwimu unaongoza kwa unyanyasaji wa kijinsia, mimba za utotoni na ndoa za utotoni, aliomba serikali kuifanya Shinyanga kama kanda maalum kwa ajili ya kudhibiti ukatili wa kijinsia.

"Asilimia 59 ya watoto walioko Shinyanga wanaolewa wakiwa chini ya umri wa miaka 18 na sielewi ni kwa nini? Sielewi ni kwa nini serikali imeamua kutumia nguvu yake kwenda kulirudisha nyuma suala la ndoa ya utotoni ambalo limeshaamuliwa na mahakama.

Tuletewe humu tubadilishe sheria lakini sasa hivi wanaenda kukusanya maoni ya wadau.

"Hii inaonyesha sisi hatuko serious. Walete sheria hapa tubadilishe na kama wanadhani kuna utaratibu umekiukwa au umekosewa tutajadili humu Bungeni, hili ndilo jumba la Watanzania! Takwimu zinaonyesha asilimia 44 ya wanawake walioko Shinyanga wananyanyaswa ndani ya ndoa zao," alisema.

**MPANGO AWEKA MSIMAMO**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema serikali inaendelea na mchakato wa kuhakikisha wanadhibiti vitendo vya mapenzi ya jinsia moja ambavyo vimeendelea kukithiri na kuathiri watoto na vijana.

Dk. Mpango alitoa kauli jana wakati akizungumza na wananchi wa Mtaa wa Buswelu katika wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza baada ya kukutana na wananchi waliobebelea mabango wakiiomba serikali kudhibiti vitendo hivyo vinavyokiuka maadili ya kitanzania.

Alisema kuwa wakati serikali ikiendelea na mchakato juu ya udhibiti wa jambo hilo, haiwezi kukubali hali ikaishia hapo na kuacha jamii ikiendelea kutafunwa na janga hilo huku akitaka jamii kuweka mkono wake ili kuzuia vitendo hivyo.

"Nimeona mmenyanyua mabango hapa, mnasema hamtaki ushoga, usagaji. Kadhalika mmesema mnaomba zitungwe sheria haraka ili kuokoa taifa. Ninyi ni watu wazuri, niwaombe nanyi wazazi wenzangu kurudi katika familia zenu kuhakikisha mnafuatilia maendeleo yao ya elimu shuleni hususani katika madaftari yao kujua wanajifunza nini," alisema.

Pia alizitaka taasisi za serikali na dini kupinga vikali matendo hayo kwa kutoa elimu na kuhubiri maadili mema kwa jamii. Pia alisema serikali itachunguza mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) hususani zile zinazopeleka maombi ya usajili serikalini ili kuhakikisha hazileti miradi yenye viashiria vya mapenzi ya jinsia moja.

**SHULE YACHUNGUZWA**

Jeshi la Polisi mkoani Njombe, limesema linafanya uchunguzi wa tuhuma za wanafunzi wa shule moja ya sekondari halmashauri ya mji Njombe kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Tunaendelea na uchunguzi na baadhi ya wanafunzi tumeweza kuwapata na tunaendelea na wana umri chini ya miaka 17 na sasa hivi kuna taratibu zingine ambazo tumewashirikisha watu wa ustawi wa jamii, mila viongozi wa dini na Tamisemi ili shule hiyo ipewe mafundisho mbalimbali yatakayosaidia hawa vijana kurudi kwenye taratibu zinazotakiwa," alisema.

**ADC YATOA NENO**

Chama cha Alliance for Democratic Change (ADC) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, kimewashauri wabunge kutunga sheria itakayokomesha ushoga na ndoa jinsia moja badala ya kulalamika bungeni.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini Iringa, Kamisha wa ADC, Daudi Masasi, alisema pamoja na mambo mazuri yanayofanywa na serikali, kuna makwazo na kilio kikubwa kwa taifa hivi ambayo ni ushoga, usagaji na ndoa za jinsia moja huku akisisitiza kuwa mwarobaini wake ni wabunge kutunga sheria kali itakayokomesha vitendo hivyo.

"Wabunge wasilalamike kama tunavyolalamika wananchi maana wao ndio wenye nafasi kubwa ya kukomesha tatizo hili kwa kulitungia sheria ambazo zitaliepusha taifa na janga hili. Kama wabunge wanalalamika ni nani atalifanyia kazi suala hili?" alihoji.

Alisema kuwa lazima wabunge wasimame kupinga hilo kwa kutunga sheria kali kama Bunge la Uganda na serikali yake ilivyopitisha sheria kali ya ushoga na ndoa za jinsia moja.

**•Imeandaliwa na Godfrey Mushi (DODOMA), Vitus Audax (MWANZA), Elizabeth John (NJOMBE) na Francis Godwin, IRINGA.**

## Sakata ununuzi Tanga Cement kaa la moto, wabunge wapinga

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WABUNGE wametilia shaka mwenendo mzima wa sakata la ununuzi wa hisa za Kampuni ya Saruji ya Tanga.

Wamesema kuruhusu Kampuni ya Saruji ya Twiga kumilikishwa hisa za kampuni hiyo wakati zinafanya biashara inayofanana, ni kutengeneza madhara makubwa kwenye upangaji wa bei na mfumuko wa bei na matokeo yake ni kumuumiza mwananchi ambaye ni mtumiaji wa mwisho.

Kutokana na ukakasi huo uliopangwa, wenye thamani ya Sh. bilioni 137, baadhi ya wabunge wamemtaka Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuingilia kati sakata hilo na kuomba marejeo ya uamuzi wa Baraza la Tume ya Ushindani (FCC) na si kuruhusu kwenda kufanya ambavyo wanafanya.

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Salome Makamba, akichangia jana mjadala wa Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka 2023/24, alisema jambo hilo linaweza kusababisha madhara kwenye upangaji wa bei kwa sababu Twiga ikiruhusiwa, itakuwa mkiritimba katika biashara ya saruji nchini kwa kuwa itakuwa na nguvu katika soko.

"Tuna jambo ambalo liko linaendelea linaweza kuleta shida kubwa ya biashara ya saruji nchini. Mwaka 2022 Twiga Cement iliomba kwenda kununua hisa za Tanga Cement na baada ya kuomba, Tume ya Ushindani, ilikwenda kufanya tathimini kama sehemu ya majukumu yake.

"Kwa sababu moja ya sifa kubwa ya kununua hisa za kampuni nyingine ambayo mnafanya biashara inayofanana hutakiwi kununua hisa kwa zaidi ya asilimia 34 ili usije ukalimiliki soko la biashara hiyo," alisema.

Kwa mujibu wa Makamba, tathmini iliyofanyika ya hisa za Tanga Cement kununuliwa na Twiga Cement, ilionekana kuna uwezekano wa Twiga Cement, kununua hisa kwa zaidi ya asilimia 68.

"Baraza limesema kwa hatari hiyo itaifanya Twiga Cement kuwa kubwa na kuifanya kumiliki soko, jambo ambalo lingeweza kuleta madhara kwenye upangaji wa bei, kwa sababu yeye ndiye mdau mkubwa kwenye eneo hilo. Ingeleta madhara makubwa kwenye mfumuko wa bei, lakini ingeleta gharama kubwa kwa mtumiaji, yaani mwananchi," alisema.

Jana asubuhi, Mbunge wa Ndanda (CCM), Cecil Mwambe, wakati anaomba mwongozo wa Spika kuhusu sakata hilo, alisema suala la Twiga Cement na Tanga Cement, likiruhusiwa litaifanya Twiga Cement kuwa na umiliki mkubwa wa soko la saruji zaidi ya asilimia 65 kwenye soko, kiasi kwamba inaweza kuifanya Twiga Cement kuamua bei ya saruji,

"Na wazalishaji wengine kwa sababu watakuwa na hisa ndogo, wakalazimishwa kupandisha bei ya saruji ili kuendana na mtu mwenye umiliki mkubwa. Ilishatolewa amri na mahakama kulipinga hili, lakini sasa hivi linaonekana linataka kurudi tena likajadiliwe kwa sababu wao bado wana 'interest' (nia) ya kutaka kununia Tanga Cement; jambo ambalo litaongeza mufumuko wa bei ya vifaa vya ujenzi," alisema.

Baadaye, Mbunge wa Singida Magharibi (CCM), Elibariki Kingu, akichangia kuhusu sakata hilo, alisema Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwa kutanguliza maslahi ya taifa, alitoa maelekezo ya kuangalia namna gani Watanzania walipita katika msukosuko mkubwa ambao ulisababisha kupanda kwa bei kubwa ya bidhaa katika nchi ikiwamo saruji.

Alisema Desemba 7, 2020, Waziri alitoa maagizo ya kufanyika utafiti wa kina ambao ungeweza kuleta majibu kwa nini Watanzania wamepata mzigo katika sekta ya ujenzi, kwa sababu ya kupanda kwa bei ya saruji.

HABARI KITAIFA

# Taasisi zapigwa 'stop' matumizi kuni, mkaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, ametoa katazo kwa taasisi zote za umma na binafsi Tanzania Bara zinazoandaa chakula na kulisha zaidi ya watu 100 kwa siku kusitisha matumizi ya kuni na mkaa ifikapo Januari 31, 2024.

Pia, taasisi zinazoandaa Chakula na kulisha watu zaidi ya 300 kwa siku zimetakiwa kusitisha matumizi ya kuni na mkaa ifikapo Januari 31, 2025.

Kutokana na makatazo hayo, serikali imeweka mkakati wa kupunguza athari za kuni na mkaa kwa kuandaa Dira ya Taifa ya Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia pamoja na mpango mkakati wa utekelezaji wa dira hiyo kwa kipindi cha miaka 10 hadi kufikia mwaka 2033.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Dk. Jafo alisema taasisi hizo zitapaswa kutumia nishati mbadala ambayo ni safi kwa ajili ya kupikia.

"Ripoti ya Tatu ya Hali ya Mazingira nchini ya mwaka 2019 inaonyesha kuwa kasi ya uharibifu wa misitu ni kubwa na kila mwaka zaidi ya hekta 469,420 huharibiwa kutokana na ukataji wa miti kwa ajili ya matumizi ya kuni na mkaa.

"Kwa mujibu wa takwimu zilizopo, inakadiriwa kuwa asilimia 16 ya ardhi imeharibika na inakabiliwa na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame kutokana na watu wengi kufanya shughuli zisizoendelevu ikiwemo kutumia nishati ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia," alisema.

Jafo aisema nishati hiyo hutumika kwa wingi kwa sababu ni rahisi kupatikana na watu wengi wanamudu gharama yake tofauti na nishati nyinginezo kama vile umeme na gesi.

"Pamoja na urahisi na unafuu wa upatikanaji wa nishati hiyo, matumizi ya kuni na mkaa yanaathiri afya ya mtumiaji kwa kusababisha magonjwa yatokanayo na kuvuta hewa chafu ambayo huathiri mapafu, moyo na pia magonjwa ya kupumua kwa watoto. Matumizi ya muda mrefu wa nishati hiyo pia husababisha magonjwa ya macho,"alisema.

Kutokana na athari kubwa za kimazingira, kiafya, kijamii na kiuchumi zitokanazo na matumizi ya kuni na mkaa kwa kupikia, alibainisha kuwa pamoja na serikali kuchukua hatua hizo watumiaji wakubwa wa nishati za kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia ni taasisi za umma na binafsi.

" Hivyo, kwa mamlaka niliyopewa chini ya Kifungu cha 13 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191, natoa katazo kwa taasisi zote za umma na binafsi Tanzania Bara zinazoandaa chakula na kulisha zaidi ya watu 100 kwa siku kusitisha matumizi ya kuni na mkaa ifikapo Januari 31, 2024.

Aidha, taasisi zinazoandaa chakula na kulisha zaidi ya watu 300 kwa siku, kusitisha matumizi ya kuni na mkaa ifikapo Januari 31, 2025,"alisema.

Alibainisha kuwa kipaumbele cha serikali kwa sasa ni kujenga uchumi wa viwanda, hivyo matumizi ya nishati mbadala ikiwamo mkaa mbadala yatatoa fursa ya viwanda vya kutengeneza mkaa mbadala sambamba na kuzalisha majiko sanifu na banifu kwa ajili ya matumizi fanisi ya nishati hiyo.

# Serikali yatangaza ajira 21,200 kada afya, elimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetangaza ajira kwa watumishi wa kada za afya na ualimu 21,200 nchini huku ikitoa onyo kwa watakaofanya udanganyifu na utapeli kuchukuliwa hatua kali za kisheria. Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, alisema Rais Samia Suluhu Hassan, ameridhia kibali cha kuajiri watumishi hao ambao kati yao kwa kada za ualimu ni 13,130 na watafundisha katika shule za msingi na sekondari kutokana na ongezeko la wanafunzi.

Alisema watumishi watakaoajiriwa katika kada za afya ni 8,070 watafanya kazi katika hospitali za halmashauri, vituo vya afya na zahanati. "Tayari dirisha la kupokea maombi kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya ajira ya TAMISEMI limefunguliwa kuanzia leo (jana) na mwisho ni Aprili 25, mwaka huu, naomba waombaji wenye vigezo wachangamkie fursa hii sifa za waombaji wanatakiwa kuwa wahitimu kutoka katika vyuo vya elimu ya juu na kati wenye fani za ualimu na afya vinavyotambuliwa na serikali," alisema.

Kairuki alisema nafasi za ajira zilizopo ni kwa wahitimu wa Stashahada, Shahada na cheti na kwa waombaji kada za elimu wanatakiwa kuwa wahitimu kuanzia mwaka 2015 hadi 2022 na kada za afya wawe wasiozidi miaka 45.

Alifafanua kuwa kwa waombaji ambao waliwahi kutuma maombi kupitia mfumo wa ajira wanatakiwa kuhuisha taarifa zao katika mfumo wa ajira.

"Asiwe mwajiriwa wa serikali au wa hospitali za mashirika ya dini ambayo tayari mshahara wake unalipwa na serikali, awe hajawahi kufukuzwa, kuacha kazi na kustaafishwa katika utumishi wa umma na kwa waombaji walioajiriwa kwa mkataba wa ajira kutoka kwa wadau wa maendeleo katika sekta ya afya waambatanishe barua za mkataba na zinazowathibitisha kutoka kwa mkurugenzi wa halmashauri husika," alisema.

Alisisitiza wawe na namba za utambulisho wa Nida, aambatanishe na nakala ya cheti cha kuzaliwa ili kuthibitisha umri huku wakipaswa kuwa tayari kufanya kazi katika halmashauri na vituo watakavyopangiwa, mashirika na taasisi zilizoingia ubia na serikali na hakutakuwa na nafasi ya kubadilishiwa kituo hadi miaka mitano iishe.

Kuhusu waombaji waliosoma nje ya nchi watatakiwa kupata namba ya ulinganifu wa matokeo kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) ili kuwawezesha kuingia katika mfumo. "Waombaji waliosoma vyuo vya nje ya nchi watatakiwa kupata ithibati ya vyeti vya kufuzu kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ili vyeti vyao vya kufuzu vitambuliwe na kupata uhalali wa kutumika nchini," alisema.

Kadhalika, alisema waombaji wenye ulemavu watatakiwa kuomba kupitia mfumo kwa kuambatanisha picha, utambulisho wa daktari kutoka hospitali na kutahadharisha watakaofanya udanganyifu hatua zitachukuliwa dhidi yao. Katika hatua nyingine, miaka mwili ya mwaka 2020/21 na 2021/2022 serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliajiri watumishi wa kada za afya 10,328 na kati ya hao Halmashauri ya Mji Nanyamba ilipata watumishi 51 wa kada mbalimbali za afya.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, akijibu swali la msingi la Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, bungeni jana, alisema serikali inatambua tatizo cla uhaba wa wataalam wa afya katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini na imeendelea kutoa vibali vya kuajiri watumishi wa kada ya afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, alisema Kituo cha Afya Majengo kilipangiwa watumishi wanne ambao ni Mteknolojia Maabara, Tabibu Msaidizi na Wauguzi wawili huku mwaka wa fedha 2022/23, serikali imepeleka vifaa na vifaa tiba katika Halmashauri ya Nanyamba vyenye thamani ya Sh. milioni 300 kwa ajili ya vituo vya huduma za afya.

Mbunge Chikota alitaka kujua mkakati wa serikali wa kupeleka watumishi na vifaa tiba katika Kituo cha Afya Majengo.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Bahati Geuzye (wa pili kulia) na Mkurugenzi wa Kampuni ya Sayarisafi, Neema Mbalamwezi, wakitiliana saini mkataba Dar es Salaam jana wa makubaliano ya kutekeleza kwa pamoja miradi ya kufikisha maji safi na salama kwa shule za msingi na sekondari kwenye mikoa mbalimbali nchini. Kushoto ni Mwanasheria wa Sayarisafi, Robinson Etuhu na (kulia) ni Meneja Elimu TEA, Mwafatma Mohamed. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mke afariki dunia ofisi ya mtendaji, alienda kuitikia wito mtalaka wake

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKAZI wa Kijiji cha Forodhani, Kata ya Sirari, Mbusiro Thomas, anadaiwa kufariki dunia katika Ofisi ya Mtendaji wa Kata ya Sirari, baada ya kwenda kuitikia wito wa aliyekuwa mume wake.

Inadaiwa kuwa baada ya kufika kwenye ofisi hizo na kupewa taarifa za hati ya wito iliyopelekwa na aliyekuwa mume wake Chacha Thomas, ambaye walitengana muda mrefu, alianguka na kuanza kutokwa jasho.

Ofisa Mtendaji Kata ya Sirari, Wakuru Mirumbe, aliwaambia waandishi wa habari jana kwamba, Thomas maarufu Wasiwasi, alifika juzi asubuhi ofisini kwake kuwasilisha hati ya wito iliyotolewa na Baraza la Ardhi Wilaya ya Tarime, ikimtaka Mbusiro kufika katika baraza hilo. Mirumbe alisema awali, Mbusiro alifika ofisini hapo na mume wake ambaye inadaiwa walitengana muda mrefu na mwanamke huyo, alifungua madai katika Baraza la Ardhi na Nyumba kwenye kata hiyo, akitaka apewe eneo la kujenga nyumba.

Alisema Baraza la Ardhi Kata lilimpa ushindi mwanamke huyo ndipo Thomas alipokata rufani kwenda Mahakama ya Ardhi na Nyumba, Wilaya ya Tarime na kuleta hati hiyo ya wito.

Alisema baada ya mwanamke huyo kufika ofisini hapo na kuelezwa alichoitiwa, kabla hajapokea barua yake, alipatwa na mshtuko na kuanguka na kuanza kutokwa jasho.

"Watu waliokuwapo hapa ofisini walijaribu kumpepea ili aamke, lakini hakuamka, tuliita polisi na walimchukua na kupelekwa Kituo cha Afya cha Sirari na uchunguzi ulipofanyika ulibaini tayari ameshafariki dunia," alisema.

Katika tukio lingine, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime Rorya, ACP Geofrey Sarakikya, alisema mpigadebe wa siku nyingi katika kituo cha mabasi Tarime Mjini, John Tall, amekutwa amefariki dunia chumbani kwake.

Alisema mpiga debe huyo amekutwa amefariki usiku wa kuamkia Pasaka huku baadhi ya wenzake wakidai kwamba huenda alikunywa pombe kupita kiasi.

HABARI KITAIFA

# Mashirika yashindwa kulipa gawio Hazina

**Na Godfrey Mushi,**
DODOMA

MASHIRIKA sita ya umma ya kibiashara yaliyopata faida, yameshindwa kulipa gawio serikalini na kusababisha kushuka kwa ulipaji wa gawio kwa mashirika na taasisi zingine za umma.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2021/22, ukaguzi wake wa mashirika ya umma 24 ya kibiashara nchini, ulibaini kuwa mashirika 12 yalipata faida na kati ya hayo, sita yalichangia na kulipa gawio kwa serikali Sh. bilioni 6.8.

Aidha, CAG amebaini kuwa taasisi sita zilizobaki zenye faida hazikulipa gawio kwa serikali, ikijumuisha benki nne ambazo zilipata faida lakini hazikulipa kutokana na kuwa na ukwasi wa mtaji kwa ajili ya kukuza uwekezaji.

Uchambuzi wa CAG katika Ripoti Kuu ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma ya Mwaka 2021/22, unaonyesha kuwa taasisi mbili zenye faida, Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KADCO) na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), zilipendekeza malipo ya gawio, lakini zilikuwa zikisubiri uidhinishwaji na wanahisa katika mkutano mkuu wa mwaka.

CAG pia amebaini taasisi zingine mbili ambazo ni Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na UTT-AMIS (Kampuni ya Dhamana ya Uwekezaji na Usimamizi wa Rasilimali Tanzania), zililipa kiasi kidogo kuliko kiasi kilichopendekezwa.

Vilevile, CAG ameeleza katika ripoti hiyo kuwa taasisi 12 zilizoripoti hasara katika kipindi hicho, hazikulipa gawio. Uwiano wa malipo ya gawio wa taasisi zenye faida, ulishuka kwa asilimia 64, ukilinganisha na mwaka uliopita 2020/21.

Kutokana na hali hiyo, CAG amependekeza taasisi zenye faida zitafute uwiano kati ya kuwekeza upya faida kwa ajili ya ukuaji na kutoa malipo ya gawio kwa wanahisa.

Pia benki za kibiashara za serikali zinapaswa kuzingatia kuboresha uwiano wa utoshelevu wa mtaji ili kuhakikisha faida ya baadaye.

Kuhusu mwenendo wa benki zinazomilikiwa na serikali na taasisi zingine za kifedha, CAG amebaini kuwa kwa mwaka 2022, Benki ya Maendeleo ya TIB, iliendelea kupata hasara kabla ya kodi ya Sh. bilioni 131.07 wakati huo huo faida ya TADB ilipungua kwa Sh. milioni 390.

Katika ripoti hiyo, CAG ameonyesha uwiano wa mikopo chechefu ya Benki ya Maendeleo ya TIB, TADB na Benki ya Azania, ilikuwa kati ya asilimia 5.86 hadi asilimia 20.32.

Pia benki hizo zote zilikuwa na jumla ya mikopo chechefu ya Sh. bilioni 278.93, ikilinganishwa na Sh. bilioni 430.61 za mwaka 2021 na kusababisha mikopo ambayo iliainishwa, ama kuwa chini ya kiwango, shaka au hasara ipatayo Sh. bilioni 357.80 iliyotolewa kwenye vitabu vya fedha.

Kwa upande mwingine, mwaka 2021 Benki ya Biashara ya Tanzania (TCB), ilikuwa na uwiano wa mikopo chechefu ya asilimia 9.87, kinyume na kiwango kinachokubalika na Benki Kuu, ambacho ni asilimia 5, huku benki hiyo ikiwa na mikopo chechefu ya Sh. bilioni 70.06.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga (katikati), akikata utepe kuzindua Ripoti ya 21 ya Haki za Binadamu Tanzania, Dar es Salaam jana.Wengine ni Ofisa Mtafiti Mwandamizi wa kituo hicho, Fundikila Wadhambi (kushoto) na Mkurugenzi wa Ujengaji Uwezo na Uwajibikaji, Felister Mauya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ripoti LHRC yabaini ukiukwaji haki tano

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimezindua Ripoti ya Haki za Binadamu 2022 inayoonyesha ukiukwaji zaidi wa haki tano, zikiwamo haki ya kuishi, haki ya usawa mbele ya sheri na haki ya elimu.

Katika taarifa iliyotolewa jana Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga ilitaja haki nyingine zilizokiukwa kuwa ni ya kuwa huru na salama na uhuru dhidi ya ukatili.

"Kwa mujibu wa ripoti hii, haki ambazo zilionekana kukiukwa zaidi mwaka 2022 ni haki ya kuishi, uhuru dhidi ya ukatili, haki ya usawa mbele ya sheria, haki ya kuwa huru na salama na haki ya elimu," alisema.

Alifafanua kuwa ripoti hiyo imegawanyika katika sura nane ikijumisha utangulizi, ilivyoandaliwa, haki za kiraia na kisiasa, haki za kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni na haki za kiujumla na haki za makundi maalum, yakiwamo ya wanawake, watoto, wazee, na watu wenye ulemavu.

Dk. Henga alitaja sura sita kuwa ni mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu, kuelezea tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti za nyuma na hitimisho na mapendekezo.

"Haki nne kati ya hizo tano, zinaangukia kwenye kundi la haki za kiraia na kisiasa, na kwamba haki hizo masuala makuu yaliyojitokeza ni pamoja na aina mbalimbali za ukatili," alisema.

Alitaja masuala hayo kuwa ni mauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina na sheria zinazominya haki mbalimbali.

"Mengine ni uhuru wa vyombo vya habari, vikwazo vya upatikanaji wa haki na changamoto ya haki jinai, ukamataji na uwekaji kizuizini kinyume na sheria, ulinzi wa taarifa binafsi, na ubambikaji kesi," alisema. Kuhusu vitendo vya ukatili, alisema tathmini inaonyesha kuwa watoto walikuwa ni wahanga wakuu wa vitendo hivyo kwa asilimia 47, wakifuatiwa na wanawake asilimia 33, wazee asilimia 10, watu wenye ulemavu asilimia nne.

Wengine ni wanaume asilimia sita na kwamba matukio ya wananchi kujichukulia sheria mkononi yameendelea kuwa mwiba kwa haki ya kuishi, ambapo kwa mwaka huo LHRC imekusanya matukio 40, ambayo ni 18 zaidi ukilinganisha na mwaka 2021.

"Ripoti pia imeangazia suala la ukatili dhidi ya watoto katika sehemu za kuabudu, ukatili dhidi ya wanawake na wasichana mtandaoni, na ukatili dhidi ya wanawake wanasiasa, ambao unakwamisha ufuatiliaji madhubuti wa haki za wanawake na wasichana," alisema.

Aidha, alisema matukio ya mauaji yanayotokana na imani za kishirikina yamepungua, lakini bado ni changamoto, hasa kwa wanawake ambao walikuwa ni asilimia 52 ya waathirika.

Alisema, mashambulio na mauaji ya watu wenye ualbino pia yameibuka upya miaka ya hivi karibuni.

Kuhusu uhuru wa kujieleza, alisema bado kuna sheria mbalimbali ambazo zina vifungu vinavyominya uhuru wa vyombo vya habari, ikiwamo Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016.

# Walalamikia utendaji polisi, wakosa imani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa dini na wananchi mbalimbali wamelalamikia utendaji wa taasisi za haki jinai likiwamo Jeshi la Polisi kuwa ni wa shaka na umefanya kukosa imani navyo.

Kutokana na hali hiyo, wametaka kufanyike mabadiliko ya kiutendaji katika taasisi zinazosimamia haki kijanai. Waliyasema hayo jana wakati wakitoa maoni mbele ya Tume ya Haki Jinai katika ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil, mjini Zanzibar.

Mchungaji wa Kanisa la Anglikana, Jackson Wambura, alisema kuna tatizo kubwa mtuhumiwa anapokamatwa na kukaa muda mrefu mahabusu lakini baadaye hugundulikana kuwa hana hatia akiwa ameshapoteza muda mwingi.

Alisema mtuhumiwa anapokaa muda mrefu mahabusu na kugundulikana kuwa hana hatia, ni vyema akalipwa fidia kwa kuwa hatua hiyo imemsababishia kutofanya shughuli zozote za kiuchumi.

"Unakuta mtu huyo aliyewekwa mahabusu kwa muda mrefu, nje ana biashara zake ambazo zinamwingizia kipato ambacho humsadia yeye na familia yake. Lakini kukaa mahabusu shughuli hizo husimama," alisema.

Kiongozi wa madhehebu ya Shia, Shaib Hussein, alisema suala la upelelezi ni donda ndugu kwa kuwa huchukua muda mrefu na kupendekeza kuwa uwapo muda maalumu ili kuondosha manung'uniko.

Alisema kutokana na upelelezi kuchukua muda mrefu, mtuhumiwa husota miaka mingi rumande na baada ya hukumu kutoka huendelea kukaa tena gerezani.

"Kama mtuhumiwa ameshakaa mahabusu miaka mitano na baada ya kesi kusikilizwa na akakutwa na hatia na kupewa adhabu ya kifungo cha miaka 10, kwa nini isijumuishwe ne ile miaka yote aliyokaa mahabusu?" alihoji.

Khamis Ali, mkazi wa Mwanakwerekwe Mkoa wa Mjini Magharibi, alisema wananchi wanakosa imani na vyombo vya dola kwa sababu havitendi haki ipasavyo.

Alisema vyombo hivyo vimekuwa vikifanya kazi kwa upendeleo kwa sababu baadhi ya watu wanaofanya makosa huachiwa huru na wingine hupewa adhabu bila kutendewa haki sawa. Nao watu wenye ulemavu, walisema bado miundombinu si rafiki kwao katika kupata huduma muhimu za kijamii.

Jamila Hamza, mmoja wa watu wenye ulemavu, alisema majengo mengi, yakiwamo ya serikali, hayajazingatia miundombinu ya watu wenye ulemavu na baadhi yao kukosa huduma muhimu katika kupata huduma.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Othman Chande, aliwasihi viongozi na wananchi kuwa huru kutoa maoni yao na nini kifanyike ili kurahisisha uboreshaji wa taasisi hizo.

## HABARI KITAIFA

# Utouh ataka mabadiliko ya Katiba ufanisi ripoti CAG

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

TAASISI ya WAJIBU imetoa mapendekezo kadhaa kwa serikali ikiwamo kufanyia marekebisho Ibara ya 143 ya Katiba ya Tanzania ili ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) iwasilishwe katika kipindi cha miezi sita badala ya tisa kama ilivyo sasa ili kuleta ufanisi.

Aidha, kupitia ripoti yake ya hali ya uwajibikaji wa masuala ya fedha na rasilimali za taifa kwa mwaka 2022, licha ya serikali kuweka wazi taarifa za fedha bado kuna udhaifu wa utoaji wa taarifa hizo kwenye serikali za mitaa na mashirika ya umma.

Akizungumza jana katika uzinduzi wa ripoti hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Mstaafu, Ludovick Utouh, alisema ripoti hiyo inatumia kigezo cha Benki ya Dunia katika kutathmini hali ya uwajibikaji kwa nchi mbalimbali.

Utouh alisema benki hiyo inapofanya tathmini na kuonekana wanafanya vibaya ni kutokana na utaratibu wa kutoa taarifa bado unaongozwa na Katiba ya Nchi ya mwaka 1977 wakati ambao mifumo ya kielektroniki ilikuwa haipo.

“Kwa sasa World Bank Public Expenditure and Financial Accountability (PEFA) inataka Ripoti ya CAG iwasilishwe kwa Rais na bungeni katika kipindi cha miezi sita lakini kwa sasa ni baada ya miezi tisa, ukienda kwenye Katiba ibara ya 143,”alisema.

Alibainisha kuwa taasisi hiyo inapendekeza kwa serikali Ibara hiyo na vifungu vya sheria vya ukaguzi wa umma vibadilishwe ili CAG awasilishe ripoti yake kwa Rais katika kipindi cha miezi sita.

“Kama mwaka wa serikali unaisha Juni 30 ikifika Desemba 31 utaratibu wote wa ufungaji hesabu na ukaguzi uwe umekamilika, hivyo tutakuwa tumepunguza miezi mitatu na faida yake kubwa ni kwamba mchakato wa bajeti kwa mwaka unaofuata utaanza wakati ripoti ya CAG imetoka na mchango katika mchakato mzima wa bajeti ya taifa.

“Imeonyesha bado kuna sehemu zina udhaifu kwa muda mrefu mfano bado bajeti ya taifa haitumiki kama msimamizi wa fedha za umma, utakuta bunge litapitisha bajeti kwa taasisi mbalimbali lakini fedha inayotoka mwisho wa mwaka utakuta haiendani na kilichoidhinishwa awali,” alisema.

“Wakati mwingine utakuta serikali ya mtaa moja imepata fedha nyingi zaidi ya mara mbili kuliko nyingine hivyo kuna kuwa na udhaifu huo wa bajeti,” alisisitiza.

Hata hivyo alisema suala la uandishi wa taarifa za fedha, ripoti hiyo imeonyesha ubora wake umeongezeka. Pia alisema pendekezo jingine ni idara ya ukaguzi wa ndani ambayo imekuwa ikipigiwa kelele mambo yasipokwenda vizuri.

Alishauri Mkaguzi wa ndani awe na ripoti mbili ambazo moja ya kiutawala na nyingine ya kiutendaji ambayo atawasilisha kwa taasisi jambo ambalo litawezesha mapendekezo kutekelezeka.

# TRA yatangaza vita bidhaa za magendo

**Na Restuta James**

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata, ametangaza vita dhidi ya wafanyabiashara haramu wa bidhaa za magendo, akieleza kutaifisha mali na vyombo vitakavyokutwa vimebeba.

Kidata alisema hayo jijini Dar es Salaam jana, alipokuwa akipokea boti mbili za kufanya doria katika ukanda wa pwani ya Bahari ya Hindi na Ziwa Tanganyika mkoani Kigoma, zilizotengenezwa na kampuni ya Amikan Ventures Limited ya nchini Dubai.

Alisema, bidhaa za magendo zinaumiza uchumi wa nchi kwa serikali kukosa mapato, viwanda vya ndani, kudumaza biashara na afya za wananchi kwa kuwa nyingine huwa ni feki.

Alitaja baadhi ya bidhaa bandia na magendo zinazoingizwa nchini kuwa ni dawa, vyakula, mavazi na vinywaji hususani pombe.

“Mamlaka imeazimia kuongeza nguvu katika eneo la doria hususani mwambao wa pwani na maeneo mengineyo nchini. Wamiliki wa vyombo vinavyotumika kusafirisha magendo kama majahazi, mitumbwi, maboti, magari, pikipiki na baiskeli waelewe kwamba vitataifishwa vikikutwa vimebeba bidhaa za magendo,” alisema.

Aliwaagiza maofisa wa Idara ya Ushuru na Forodha wa TRA, kushirikiana na vyombo vingine vya dola pale wanapokabiliana na wahalifu wa magendo.

Naibu Kamishna wa Forodha na Ushuru wa bidhaa, Godfrey Kitundu, alisema vitendo vya magendo vimeongezeka kwa asilimia 70.3 katika kipindi cha Julai hadi Desemba, mwaka jana, ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2021.

Alisema mwaka jana idara yake ilifanikiwa kukamata bidhaa za magendo zenye thamani ya Sh. bilioni 11.05, wakati mwaka juzi walikamata bidhaa hizo zenye thamani ya Sh. bilioni 7.77.

Alisema TRA inakusudia kununua boti nyingine tano za doria ambazo zitapelekwa katika mikoa ya Pwani, Lindi, Mtwara, Rukwa na Mbeya.

Hata hivyo, alisema TRA ina boti 11 za doria ambazo mbili kati ya hizo ni chakavu na tatu zinahitaji matengenezo makubwa.

Mshauri wa ununuzi wa kampuni ya Amikan Ventures Limited, Milton Shango, alisema boti hizo zimekaguliwa na wataalamu wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) pamoja na Chuo cha Bahari Dar es Salaam; na kuthibitishwa ubora na usalama wake.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA WA MIZANIA ULIOKAGULIWA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa Sasa 31 Desemba 2022 | Mwaka Uliopita 31 Desemba 2021 |
|---|---|---|---|
| A | **ASSETS** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 595.79 | 832.82 |
| 2 | Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 4,942.86 | 9,467.90 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za serikali | 43,769.98 | 35,070.14 |
| 4 | Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 504.40 | 529.37 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 0.04 | 141.50 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0.00 | 0.00 |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | 0.00 | 0.00 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0.00 | 0.00 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 4,179.14 | 36,356.91 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0.00 | 0.00 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 50,045.18 | 51,115.39 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,347.58 | 1,069.55 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0.00 | 0.00 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0.00 | 0.00 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,149.36 | 726.37 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **106,534.34** | **135,309.96** |
| B | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 9,984.60 | 36,430.00 |
| 18 | Amana za Wateja | 53,334.13 | 56,654.61 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0.00 | 0.00 |
| 20 | Amana Maalumu | 0.00 | 0.00 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0.00 | 0.00 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 0.00 | 0.00 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,652.44 | 1,533.45 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0.00 | 0.00 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0.00 | 0.00 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 0.00 | 0.00 |
| 27 | Dhima Nyingine | 921.31 | 453.03 |
| 28 | Madeni | 0.00 | 0.00 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **65,892.48** | **95,071.09** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29*** | **40,641.86** | **40,238.87** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 467.69 | 1,279.37 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 6,448.73 | 3,516.20 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 895.43 | 2,613.31 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 0.00 | 0.00 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0.00 | 0.00 |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **40,641.86** | **40,238.87** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 6,747.30 | 6,760.70 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 2,181.49 | 1,632.81 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 80.66 | 437.92 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 0.00 | 0.00 |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 38.15% | 29.74% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4.35% | 3.17% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 79.15% | 55.42% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 46.98% | 37.78% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 92.46% | 90.96% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -31.98% | 14.57% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -21.27% | 11.30% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI ILIYOKAGULIWA KWA MWAKA UNAOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa Sasa 31 Desemba 2022 | Mwaka Uliopita 31 Desemba 2021 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 8,707.52 | 9,635.81 |
| 2 | Gharama za Riba | 3,258.97 | 3,237.67 |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,448.54** | **6,398.15** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 6.13 | 0.00 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 951.18 | 73.77 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **703.93** | **945.99** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 196.93 | 152.73 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 507.00 | 792.38 |
| | 6.3 Gawio | 0.00 | 0.00 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 0.00 | 0.87 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **3,839.70** | **3,529.20** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 1,633.82 | 1,376.29 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 34.07 | 33.92 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 2,171.82 | 2,118.99 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,355.47** | **3,741.16** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 460.03 | 1,127.85 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **895.43** | **2,613.31** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | 26 | 25 |
| 12 | Mapato kwa Hisa | 27 | 80 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 27 | 80 |
| 14 | **Idadi ya Matawi** | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.76% | 2.09% |
| (II) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.19% | 6.70% |
| (III) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 62.41% | 48.05% |
| (IV) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.04% | 5.52% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA ILIYOKAGULIWA KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa Sasa 31 Desemba 2022 | Mwaka Uliopita 31 Desemba 2021 |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 895.43 | 2,613.31 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | 0.00 | 0.00 |
| | Hasara katika mali | 1,371.25 | 402.48 |
| | -Badiliko halisi katika Mikopo | 95.22 | -2,690.54 |
| | Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | 0.63 | 0.00 |
| | Mabadiliko halisi katika Amana | -29,765.88 | 11,835.71 |
| | Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | 0.00 | 0.00 |
| | Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 193.30 | 715.81 |
| | Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | 807.91 | 761.66 |
| | Kodi iliyolipwa | -700.82 | -1,168.25 |
| | Mengineyo(bainisha) | 0.00 | 0.00 |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **-27,102.95** | **12,470.18** |
| II | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | |
| | Gawio lililopokewa | 0.00 | 0.00 |
| | Ununuzi wa Mali za kudumu | -148.55 | -5.82 |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | 9.03 | 0.00 |
| | Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | -7,000.05 | -2,005.73 |
| | Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | 0.00 | 0.00 |
| | Mengineyo(bainisha) | 0.00 | 0.00 |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **-7,139.57** | **-2,011.55** |
| III | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0.00 | 0.00 |
| | Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0.00 | 0.00 |
| | Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0.00 | 0.00 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | -492.45 | 0.00 |
| | Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | 0.00 | 0.00 |
| | Mengineyo(Malipo ya dhima kukodishwa)-IFRS 16 | -280.53 | -254.15 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **-772.98** | **-254.15** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | |
| | Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **-35,015.50** | **10,204.48** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa mwaka | 47,101.31 | 36,896.83 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa mwaka** | **12,085.81** | **47,101.31** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI ILIYOKAGULIWA KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 32,830.00 | - | 6,129.50 | 1,279.37 | - | - | **40,238.87** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 895.43 | - | - | - | **895.43** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (492.45) | - | - | - | **(492.45)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 811.68 | (811.68) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **32,830.00** | **-** | **7,344.16** | **467.69** | **-** | **-** | **40,641.86** |
| **Mwaka Uliopita 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 32,830.00 | - | 4,754.21 | 41.35 | - | - | **37,625.56** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,613.31 | - | - | - | **2,613.31** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,238.02) | 1,238.02 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **32,830.00** | **-** | **6,129.50** | **1,279.37** | **-** | **-** | **40,238.87** |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2022**

Taarifa ya fedha hapo juu ni sehemu ya Taarifa kuu ya fedha ya Canara Bank Tanzania Limited kwa kipindi cha fedha kinachoishia tarehe 31 Desemba 2022, ambayo imeandaliwa kwa kufuata viwango vya kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha(International Financial Reporting Standards(IFRS)). Taarifa hii ya fedha ilikaguliwa na wakaguzi wa nje waitwao Nexia SJ Tanzania na kupata hati safi.


| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | MKURUGENZI MKUU | (IMESAINIWA) | 11-04-2023 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (IMESAINIWA) | 11-04-2023 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (IMESAINIWA) | 11-04-2023 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi.**

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (IMESAINIWA) | 11-04-2023 |
| MWANAIDI A MTANDA | MKURUGENZI | (IMESAINIWA) | 11-04-2023 |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII




## Maofisa benki wapewe elimu kuhudumia wenye ulemavu mikopo

**SHIRIKISHO** la Vyama la Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), limelalamikia taasisi za fedha zinazobeba dhamana ya kutoa mikopo kuhusu elimu duni kwa maofisa wake na kusababisha kundi la watu wenye ulemavu kutopewa kipaumbele wanapohitaji mikopo benki.

Kundi hilo limedai baadhi ya benki kuwanyanyapaa, kutokana na maofisa wake kutokuwa na elimu ya kuwasaidia watu hao na haki zao katika kupata huduma bora zenye usahihi kwa kundi hilo.

Kundi hilo limebeba watu wenye ulemavu wa aina mbali mbali, kuna wengine wasioona, wasiosikia (viziwi) na wasioweza kuongoea (bubu), hivyo ni lazima wafikiriwe kwa kupatiwa huduma sahihi kulingana na ulemavu wao.

Katibu Mkuu wa SHIVYAWATA, Jonas Lubago, anasema katika Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022, iliyowasilishwa bungeni, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, alisema amebaini mamlaka 180 za serikali za mitaa hazikukusanya mikopo.

Mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ya Sh. bilioni 88.42 haikukusanywa kutokana na kutokuwapo kwa ujuzi wa kutosha kwenye Idara ya Maendeleo ya Jamii.

Idara hiyo ngazi ya mamlaka ya serikali ya mitaa haikuwa na ujuzi wa kutosha kufanya upembuzi yakinifu kwa vikundi vilivyoomba mikopo, kuvisimamia katika kufanya urejeshaji wa mikopo na kutoa mafunzo ya biashara kwa wanufaika.

"Kati ya kiasi hicho Sh. bilioni 2.25 zinahusu vikundi vilivyoacha shughuli za biashara na kuleta mashaka juu ya urejeshwaji wa mikopo hiyo, pia nilibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa zilitoa Sh. milioni 895.94 kwa vikundi 48 ambavyo havikuwapo," alisema CAG Kichere.

Katika wasilisho la CAG, Rais Samia Suluhu Hassan, fedha za mikopo inayotolewa na halmashauri zipatazo 180 nchini, zimegeuka kuwa kichaka, kwa kuwa ndiko chanzo cha upotevu wa fedha za serikali, akipendekeza mabadiliko yafanyike na sasa itolewe benki.

Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorejewa 2019), kwa kuongeza kifungu cha 37A mahususi kwa ajili ya kuwezesha mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; Kifungu cha 37A (1) cha sheria hiyo kinazitaka halmashauri zote kutenga asilimia 10 ya mapato yao ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilivyosajiliwa.

Vilevile, Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, 2019 (Tangazo la Serikali Na. 286 la 5/04/2019) zinataka mamlaka zote za serikali za mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Katibu wa SHIVYAWATA anafafanua kuwa utaratibu uliokuwa unatumika siku zote ulifuata kanuni iliyotolewa na TAMISEMI (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa). "Hatujajua masharti yatatumika yapi, ya kibenki au Tamisemi."

"Na kama tutatumia masharti ya kibenki kwakuwa lengo ni mikopo irejeshwe, shaka litabakia kuwa uwezo wa WWU (Watu Wenye Ulemavu) kutimiza masharti hayo.

Wakati mikopo ikitolewa kwenye halmashauri maana yake huduma hiyo ilishuka hadi ngazi ya kata, jirani na makazi ya wakopaji.

Hata hivyo, kukosekana miundombinu rafiki kwa baadhi ya watu wa kundi hilo, kunahitajika marekebisho na ukarabati wa majengo ili WWU waweze kuyafikia kwa urahisi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



Na Christina Mwakangale

### Muungwana Lazima Nilonge

## Kukosekana taa darajani Stendi ya Magufuli ni kuwahatarisha wateja

**UNAPOTAJA** Kituo cha Mabasi cha Magufuli kilichopo Mbezi, mkoani Dar es Salaam, kina kazi ya kutoa huduma za safari ziendazo mikoani na nchi jirani, huku kikitajwa kuwa na hadhi ya kimataifa.

Hiyo inatokana na uhalisia wa huduma inazotoa kwa siku, abiria wanasafiri kwa 'ruti' tofauti kwenda maeneo tofauti na mabasi yanayokadiriwa wastani wa 200 kwa siku.

Kwa sasa unapoingia au kutoka kwenye kituo hicho kwa abiria wanaotembea kwa miguu, inawalazimu kupita njia ya daraja la juu, ili kuwapa usalama watumiaji wa kituo hicho hususan abiria.

Na inapokuwa jioni giza limeingia, mara moja utaona kasoro kwamba, kuna giza kwenye daraja hilo, hasa kwa watumiaji wa usiku. Hapo inaangukia mara moja changamoto, kwa kuwa wanaolitumia iwe ni watu wenye ulemavu, wazee, watoto na makundi mengine ni hatari kwao.

Hata kwa usalama, pia unakuwa mdogo, ikizingatiwa kwamba juu ya daraja kumezungukwa na wapiga debe ambao wao kazi yao ni kushawishi abiria watumie usafiri wao, lakini nani anajua kwamba wote kazi yao ni hiyo.

Iko bayana, watu wasio na nia nzuri siku zote wanapenda kutumia mazingira ya aina hiyo, hata wakatekeleza azma zao mbaya kwa manufaa yao, ikizingatiwa abiria wengi wanakuwa wamebeba vitu vyenye thamani.

Kwenye msafara wa mamba na kenge wamo, huo ni msemo wa Waswahili ambao naweza kuutumia hapa, kwa kuwa wapiga debe hao mbali na kukatazwa na mamlaka husika kufanya hivyo, kuna ushahidi unaotolewa mara kadhaa kwamba wapo na vibaka.

Uwapo wa giza kwenye daraja hili isiwe fursa kwa watu wenye nia ovu na kutaka kuutumia mwanya huo kwa kuleta usumbufu kwa watumiaji hasa abiria.

Kama ambavyo inafahamika kwamba matumizi ya kituo hicho ni saa 24, kwa kuwa wapo wasafiri wanaotoka kanda mbalimbali ikiwamo ya Ziwa ambao huwasili kituoni zaidi ya saa sita usiku.

Mazingira rafiki ya kituo hicho yakifanyiwa uangalizi yanatosha kukifanya kituo hicho kuwa salama kwa mtu yeyote na hasa wageni, tena kwa majira yoyote, iwe mchana au usiku, kwa kuwa ni wakati wa mamlaka husika kuzingatia uwapo wa taa eneo hili.

Wakati mazingira ya watumiaji kituo hicho yanawalazimu abiria kupita juu ya daraja, ni vyema eneo liwe na uhakika wa kutumika kwa madhumuni yaliyotumika kulijenga kuwa daraja. Kuna haja kwa namna zote mahali hapo pakawekwa taa, huku watu ambao wanapageuza eneo hilo kijiwe, wapigwe marufuku na daraja litumike kwa hitaji lake.

Nijuavyo kwa ilivyo sasa, matumizi ya taa sio ya gharama, kwa kuwa zipo zilizoundwa kwa kutegemea chanzo cha jua mchana kutwa, kisha usiku taa zikawashwa bila gharama ya umeme utokanao na wazalishaji umeme Tanesco.

Pia, daraja hilo lifanyiwe usafi kwa kuwa mara kadhaa usafi huwa duni, hujaa mchanga, taka za plastiki na makaratasi, uchafu ambao unashusha hadhi ya kituo hicho ambacho ni taswira ya mkoa na nchi kutokana na kupokea wageni wanaotoka nchi jirani kila uchao.

Kituo hicho kilizinduliwa Februari mwaka 2021 na Hayati John Magufuli, huku kikiwa na uwezo wa kuhudumia mabasi 3,456 kwa siku, abiria 224,000 kwa siku na kuegesha magari madogo zaidi ya 280 na kuegeshwa mabasi 1000 wakati wa usiku.

Kadhalika, ofisi za benki, huduma za simu, hoteli, ofisi za wahusika uhamiaji, maduka pamoja na eneo la kupumzikia abiria na maliwato ni kati ya huduma muhimu zinazopatikana kituoni hapo. Najiuliza, kwanini hatupati uwiano katika hitaji la darajani kwa thamani hiyo stahiki?

# Aliyeshtakiwa kujipatia bil. 5/- za upatu aachiwa huru

**Na Grace Gurisha**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kampuni ya JATU Public Ltd, Peter Gasaya (32), anayetuhumiwa kujipatia fedha za Upatu, Sh. bilioni 5.1 kwa njia ya udanganyifu, ameachiwa huru na mahakama, baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), kuwasilisha hati mahakamani ya kutokuwa na nia ya kuendelea na mashtaka dhidi yake.

Gasaya kwa mara ya kwanza alipandishwa kizimbani Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam Desemba 29, 2022 kwa tuhuma za kujipatia kiasi hicho cha fedha kutoka Saccos ya JATU kwa madai kuwa ataizalishia faida huku akijua sio kweli.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mrio wa mahakama hiyo kuwa kesi iliyetwa kwa ajili ya mshtakiwa kusomewa maelezo ya awali (PH), lakini DPP hana nia ya kuendelea na mashtaka dhidi yake.

"DPP amewasilisha hati ya kutokuwa na nia ya kuendelea na mashtaka dhidi ya mshtakiwa chini ya kifungu namba 91 (1) cha Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA)," alidai Wakili Mwanga.

Hakimu Mrio alikubali na ombi hilo chini ya kifungu hicho na kumuachia huru mshtakiwa huyo, baada ya kusota gerezani tangu Desemba 29, mwaka jana.

Ilidaiwa kuwa kati ya Januari Mosi, 2020 na Desemba 31, 2022, mshtakiwa akiwa ndani ya jiji na Mkoa wa Dar es Salaam na Mkurugenzi wa kampuni hiyo alijipatia Sh. 5,139,865,733 kwa njia ya udanganyifu kutoka JATU Saccos.

Mshtakiwa alichukua fedha hizo kwa madai kuwa atazipanda fedha hizo na kuzalisha faida huku akijua sio kweli.

Mshtakiwa aliposomewa shtaka lake, alikana kuhusika na tuhuma hizo. Hata hivyo, alishindwa kutimiza masharti ya dhamana kwa madai kuwa fedha iliyotajwa ya dhamana ni kubwa kwake.




Ofisa Mazingira na Uendelevu wa Taasisi ya Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (Pass Trust), Oscar Munga akifafanua jambo kwa waandishi wa habari, mjini Mtwara juzi, kuhusu umuhimu wa kufanya kilimo biashara chenye tija kwa mazingira ili kuchochea ukuaji wa kilimo endelevu mkoani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kifua kikuu chatesa watoto Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATOTO 90 mkoani Njombe wameathirika na kifua kikuu (TB) kwa kipindi cha mwaka 2021, kati yao wawili wakifariki dunia kwa sababu ya kuchelewa kufikishwa hospitali.

Akizungumza na Nipashe, Mratibu wa kifuu kikuu na ukoma Njombe, Dk. Mashaka Matanga, alisema kuna kifua kikuu cha aina mbili, cha ndani na nje mapafu.

"Kifua kikuu cha ndani ya mapafu ndiyo kinachoambukiza kwa wakubwa na wadogo na kifua kikuu cha nje ya mapafu hakiambukizi kwa njia ya hewa kwa sababu kinakuwa kimeingia maeneo ambayo yanamuathiri mgonjwa husika," alisema Matanga.

Alisema kuwa takwimu za ugonjwa wa kifua kikuu ni kubwa ikilinganishwa na jinsi janga lilivyo.

"Maana yake kama mkoa kwa ujumla tunapata wagonjwa watu wazima na watoto zaidi ya 1,000 na kwa watoto zaidi ya 100 maana yake janga hili ni kubwa kwa watoto inahitaji mikakati ya kulishusha na kulipoteza kwa sababu kimkakati na kisera katika nchi yetu ni kuondoa kifua kikuu katika jamii," alisema Matanga.

Alisema kunahitajika kuwekwa mikakati ya uibuaji wa wagonjwa na kuwatibia kwa wakati ili kupunguza na kuepusha ugonjwa huo kuzidi kuenea katika jamii.

"Moja ya dalili ya kifua kikuu kwa watoto ni pamoja na mtoto kushindwa kuongezeka uzito au kupungua uzito, dalili nyingine ni mtoto kuwa na shida ya lishe au udumavu na amewahi kutibiwa zaidi ya wiki nne bila ya haueni yoyote, dalili nyingine zinafanana na ugonjwa unaitwa nimonia, muda mwingine mtoto anapata homa mara kwa mara na anapotibiwa kwa dawa za hospitalini anakuwa hapati haueni yoyote," alisema.

Aliwaasa wazazi wanapoona mtoto anapopata shida ya kikohozi au homa za mara kwa mara, kuchemka, kifua cha kubana, anahitaji kufika kwenye vituo vya kutolewa huduma za afya.

Mratibu wa kifua kikuu Wilaya ya Makete, Dk. Jonathan Kitundu, alisema tatizo la kifua kikuu kwa watoto lipo na katika jamii watu wanaoweza kuwabaini kuwa na kifua kikuu ni asilimia 15. Alisema watoto kinga zao zinapanda na kushuka kwa sababu ya umri wao na kuwa rahisi kupata maambukizi.

"Watoto hawa wadogo mara nyingi sana ni ngumu kupata sampo ya kupima makohozi yao hivyo unakuja kukuta mtoto anatibiwa kama ugonjwa wa nimonia au kikohozi sugu, lakini kumbe ni kifua kikuu tu, kwa hiyo sasa mapokeo ya mtindo huu, mtoto anaumwa kifua kikuu wanafikiria zaidi mtoto anaumwa nimonia," alisema.

Pia, aliitaka jamii kuwa na utaratibu wa kutafuta tiba za afya zaidi kuliko kutegemea mbadala wakiwa nyumbani.

"Mara nyingi wanaanzia kwa tiba mbadala, lakini wakizidiwa ndiyo wanakuja kuwaleta hospitali, kama watu wazima wanafanyiwa hivyo basi na watoto bado wanafanyiwa hivyo na wengine huenda wanapoteza maisha kwa sababu amepelekwa kwenye tiba mbadala badala ya kumleta hospitali," alisema Kitundu.

# TANROAD kutekeleza miradi 16 ya barabara

**Na Gwamaka Alipipi**

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS), umesema tangu kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22 unaendelea kutekeleza miradi 16 yenye thamani ya Sh. trilioni 1.4 nchini.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Rogatus Mativila, alibainisha hayo juzi jijini Dar es Salaam, wakati wa ukaguzi wa mradi wa barabara ya mabasi yaendayo haraka awamu ya tatu, inayoanzia katika Barabara ya Nyerere hadi Gongo la Mboto (km.23.3) kwa gharama ya Sh. bilioni 231.

Mhandisi Mativila alisema mradi huo unatarajia kukamilika Machi mwakani na kwa sasa umefikia asilimia tano na mkandarasi Kampuni ya Sinohydro anaendelea na ujenzi.

"TANROADS kazi yetu ni kujenga barabara, kila mwaka wa fedha unapoingia tumekuwa tukitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara nchi nzima, kwa mwaka wa fedha 2021/22 miradi 16 ilitengewa Sh. trilioni 1.4. Hata mwaka wa fedha 2022/23 kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa miradi itakayoanza kazi mwakani, " alisema Mativila.

"Sisi hatulipi fedha bali tunapeleka certificate (cheti) Wizara ya Fedha ambao wao ndiyo wanamlipa mkandarasi. Na Mkandarasi analipwa kulingana na ufanisi wa kazi aliyoifanya."

Kuhusu mradi wa barabara ya mabasi yaendayo haraka awamu ya tatu, Mhandisi Mativila alisema ujenzi huo utakuwa wa njia sita hali itakayo punguza msongamano wa magari katika barabara hiyo.

Alisema mradi huo utakamilika Machi mwakani, utajengwa kwa kiwango cha zege ikiwa ni mpango wa serikali katika kukabiliana na foleni barabara za jiji la Dar es Salaam.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Dar es Salaam, Harun Senkuku, alisema ujenzi wa mradi huo ulianza Januari mwaka jana, kwa sasa mkandarasi anaendelea na ujenzi wa barabara za kati pamoja na vituo.

Alisema mradi huo utakapokamilika utakuwa na vituo 32, kwa sasa ujenzi wa vituo saba umeshaanza na kilometa mbili za barabara zimeshajengwa.

Senkuku alisema mradi huo pia utahusisha ujenzi wa vituo 32, karakana moja, vituo vikubwa vinne na daraja kubwa moja.

# Mshindi wa SBL akabidhiwa gari

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL), imekabidhi gari jipya aina ya Toyota IST kwa Shamimu Mushi, mkazi wa Arusha, aliyeshinda katika droo ya mwisho ya promosheni ya bia ya Pilsner Lager inayojulikana kama "Kapu la Wana".

Akizungumza jana katika hafla ya kukabidhi zawadi hiyo iliyofanyika kwenye baa ya The Blue jijini hapa, Meneja Masoko wa SBL Kanda ya Kaskazini, Andrew Msiagi, alisema walifika katika eneo hilo kwa ajili ya makabidhiano ya zawadi hiyo ya gari.

"Tumemaliza kampeni ya Kapu la Wana na nina furaha zaidi kwa mwanamke kuibuka mshindi wa mwisho wa kampeni yetu,hii inaonyesha kuwa chupa yetu ya Pilsner inapendwa na watu wa kila aina," alisema.

Msiagi alisema promosheni hiyo ilianzishwa kwa lengo la kuwazawadia watumiaji wa bia hiyo, wanaofanya kazi kwa bidii katika Kanda za Ziwa, Kusini na Kaskazini ili kuwasaidia kubadili maisha yao kwa namna moja au nyingine kwa kuwa kuwazawadia zawadi mbalimbali zikiwamo simu janja na pikipiki.

"Kupitia promosheni hiyo, SBL iliwekeza Sh. milioni 36 na washindi 22 walijishindia zawadi mbalimbali katika kipindi cha miezi miwili ya promosheni.

"Washindi walikuwa kutoka kanda za Ziwa,Kusini na Kaskazini ambako promosheni ilikuwa ikitekelezwa na zawadi hizo ni pamoja na simu janja,televisheni,pikipiki na gari kama zawadi kuu," alisema.

Mshindi wa gari hiyo, Shamimu Mushi, alisema amefurahi kuibuka mshindi wa gari jipya baada ya kushiriki katika droo ya pr0mosheni hiyo ya bia ambayo ni chaguo lake.

"Sikutarajia kushinda zawadi hii. Naishukuru SBL kwa kuanzisha promosheni hii na kunizawadia zawadi ambayo itabadilisha maisha yangu," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika tukio hilo, alipongeza SBL kwa kuandaa promosheni hiyo iliyowapa fursa ya kurudisha kidogo kwa jamii.

"Naipongeza SBL kwa mpango huu,kupitia promosheni hii imemwezesha mwanamke ambaye leo anaondoka na gari jipya ambalo naamini litabadili maisha yake yatakuwa bora kuanzia hapa na kuendelea," alisema.

# Ofisa elimu aonya matumizi teknolojia

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

KAIMU Ofisa Elimu Mkoa wa Arusha, Emanuel Mahundo, amesema licha ya kukua kwa teknolojia na kuwa nzuri, ikitumika vibaya inaweza kueneza tabia zisizofaa katika jamii endapo itatumika kwa dhamira isiyokusudiwa.

Kadhalika, ametoa rai kwa jamii kutumia ukuaji wa teknolojia vizuri kama kutangaza shughuli zao wanazofanya kwa ajili kukuza uchumi wao. Aliyasema hayo jana wakati wa kongamano la mashindano ya teknolojia yaliyoandaliwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya E3Empower yaliyofadhiliwa na Serikali ya Korea kupitia shirika lake la misaada la kimataifa la KOICA.

Mahunda alisema teknolojia ni kichocheo cha maendeleo katika nyanya mbalimbali lakini isipotumiwa vizuri, inaweza kusababisha madhara ikiwamo kuharibu utamaduni wa nchi.

Aidha, kaimu ofisa elimu huyo aliwataka wanafunzi kutumia teknolojia kwa mtazamo chanya na si vinginevyo. Pia aliwaonya kuacha kuiga kila kinacholetwa na teknolojia hiyo.

"Kama mkoa tunasisitiza ngazi ya shule na kwa wazazi kuwa makini na watoto katika kutumia hii mitandao ya kijamii kwa kuwa tumeshaona inatumika vibaya na vijana wetu na matumizi yote tuliwaelekeza waalimu kudhibiti," alisema Mahundo.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema kati ya halmashauri saba za mkoa huo, ni halmashauri tano zinafunisha soma la teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kwa ajili ya kusaidia wanafunzi kusoma kwa urahisi. Alisema kwa kuwa teknolojia inarahisisha ufundishaji shuleni.



Mkuu wa Kituo cha Polisi Orkesumet, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, SP Christina Mkonongo akitoa elimu ya polisi jamii, ulinzi shirikishi na kupiga vita mmomonyoko wa maadili kwa wakazi wa Mji mdogo wa Mirerani juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mbunge agawa mabati, saruji ujenzi makazi ya katibu UWT

**Na Allan Isack,** BABATI

MBUNGE wa Viti Maalum wa Mkoa wa Manyara kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Regina Ndege, ametoa msaada wa mabati 20 na mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Katibu wa Umoja wa Wanawake wa Tanzania (UWT) Wilaya ya Babati Vijijini.

Mbunge huyo, amekabidhi vifaa hivyo vya ujenzi baada ya hivi karibuni kutoa ahadi ya kuwapa vifaa hivyo vya ujenzi alipotembelea eneo hilo.

Vifaa hivyo alivikabidhi jana mbele ya Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Babati Vijijini, Katibu wa UWT Babati wa wilaya hiyo, madiwani wa viti maalum na wajumbe kamati ya utekelezaji wa UWT wa wilayani humo.

Aidha, alitumia fursa hiyo, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kufanikiwa kutekeleza ahadi aliyoitoa alipoafanya ziara ya kutembelea eneo hilo na aliahidi kuwapa vifaa hivyo vya ujenzi wa nyumba hiyo.

"Namshukuru Mungu kwa mimi kufanikiwa kutekeleza ahadi yangu niliyoitoa kwenu na kwa moyo thabiti nawapongeza wale wote mliofika kushuhudia tukio hili," alisema ndege.

Katibu wa UWT Wilaya ya Babati Vijijini, Tupilike Kalibenjela, alimshukuru mbunge huyo kwa kukamilisha ahadi aliyoitoa kwa wanawake wa eneo hilo kwa kukabidhi vifaa hivyo.


"Waswahili husema ahadi ni deni, hivyo mbunge wetu ameonyesha uungwana kwa kutimiza ahadi hiyo hivyo wanawake wa Babati Vijijini wanamshukuru mno," alisema Kalibenjela.

Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa CCM kupitia Wilaya ya Kiteto, Sisca Seuta, alimpongeza Ndege kwa kukamilisha ahadi hiyo ambayo aliwaahidi wanawake hao.

"Regina wewe ni maana halisi ya Mbunge wa Viti Maalum, uko pamoja na wananchi na wanawake wote wa mkoa wa Manyara, bila kubagua kweli tunajivunia wewe," alisema Seuta.

Mjumbe wa UWT Wilaya ya Simanjiro, Jacqueline Momo, alisema mbunge huyo anatekeleza ahadi zake, hivyo atakaa kwenye kiti hicho cha ubunge hadi achoke mwenyewe.

"Mbunge usiyekuwa na majivuno wala hauringi, hufungi vioo kwenye gari,unasikiliza kila mtu na kupokea simu kila wakati, umeacha alama Manyara,wacha watu tukusemee wewe ni mfano wa kuigwa," alisema Momo.





# Wachimbaji wadogo wajenga vyoo kupambana na maradhi

**Na Marco Maduhu,** GEITA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu katika machimbo ya Nyamatagata yaliyoko Kata ya Mgusu Halmashauri ya Geita Mji, wamejenga vyoo katika maeneo ya machimbo ikiwa ni sehemu ya kudhibiti magonjwa ya milipuko yanayodaiwa kuwa hatari katika machimbo hayo.

Inaelezwa kuwa katika machimbo hayo, watu wamekuwa wakijisaidia ovyo vichakani hali ambayo imekuwa ikisababisha milipuko ya magonjwa ya mara kwa mara na kuathiri utandaji kazi wao .

Baadhi ya viongozi wa machimbo hayo mkoani Geita, walioambatana na timu ya wanasheria watetezi wa mazingira kwa vitendo (LEAT) kuona hali ya usafi na utunzaji wa mazingira katika eneo hilo, walisema hali hiyo imeboresha usafi na usalama wa kiafya kwa wachimbaji hao.

Mmoja wa viongozi kwenye mgodi huo, Boniphace James, alisema machimbo hayo yalianza Mei 20, mwaka jana, na kulikuwa na watu wengi takribani 20,000 na walikuwa hawana sehemu ya kujisaidia zaidi ya vichakani na kwenye vyanzo vya maji.

"Machimbo haya ya Nyamatagata awali hali ya usafi ilikuwa mbaya sana. Tunamshukuru Mungu hatukupata magonjwa ya mlipuko vinginevyo watu wengi wangekufa sana. tulikaa na kuamua kujenga vyoo pamoja kuwabana watu wenye leseni nao wajenge vyoo. Kwa sasa hali ya usafi ni nzuri," alisema James.

Mwenyekiti katika machimbo hayo, Elias Lukanya, alisema mbali na ujenzi wa vyoo pia wameajiri kampuni ya Makambaya Investment, ambayo kila siku inakusanya uchafu wote ambao unazalishwa kwenye machimbo na kupeleka dampo ili kuhakikisha hali ya usafi inaimarika.

Ofisa Mazingira Mkoa wa Geita, Tito Mlelwa, aliupongeza uongozi wa machimbo hayo kwa kusimamia usafi na utunzaji wa mazingira, huku akiahidi suala la kujengewa vyoo na serikali atalifikisha sehemu husika.

Naye Valeria Macha kutoka LEAT, alisema wamekuwa wakitoa mafunzo kwa viongozi mbalimbali juu ya usimamizi wa rasilimali za nchi na kufanya uchimbaji wa madini bila ya kuathiri mazingira.

# Wachimbaji wadaiwa kufukiwa wakichimba madini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu katika mgodi wa Mwime kata ya Zongomela, Kahama mkoani Shinyanga, wanadaiwa kufukiwa na kifusi wakiwa katika uchimbaji wa madini kutokana na mvua za masika zinazoendelea kunyesha katika eneo hilo.

Mgodi huo ulioko katika bonde kubwa la maji na mvua zinaponyesha eneo hilo linajaa maji na kusababisha baadhi ya mashimo yanayosadikiwa kuwa na dhahabu, kusitisha uchimbaji au uzalishaji kwa muda mpaka maji yatakapovutwa kwa kutumia mitambo na wale wanaoingia bila kuchukua hatua wanafukiwa.

Meneja wa Mgodi huo, Joseph Nalemi, aliwaambia waandishi wa habari juzi kuwa wakati mvua zinaendelea kunyesha kuna baadhi ya wachimbaji walikuwa wanaendelea na uchimbaji katika eneo hilo na mpaka sasa hawajafahamika na hawaonekani wakirejea.

Alisema, bado wanaendelea na uokoaji kwa kushirikiana na Jeshi la zimamoto na Uokoaji huku mvua zikiendelea kunyesha na maji yakiendelea kujaa ndani ya mashimo na tangu Machi 27, mwaka huu, walipoanza uokoaji, mpaka sasa hakuna mafaniko yoyote waliyopata ya kupata mwili hata wa mchimbaji mmoja.

Nalemi alisema, wanatarajia kusitisha uokoaji baada ya eneo hilo kuendelea kujaa maji kwa kuwa hakuna uhakika kuwa ndani ya mashimo hayo kuna wachimbaji wadogo waliofukiwa kwa sababu mashimo hayo yalikuwa yametelekezwa kwa muda mrefu.

"Shughuli za kufuatilia watu waliofukiwa zilianza baada ya taarifa kutufikia kuwa baadhi watu wamefukiwa mashimoni. Tulichukua hatua za haraka za kuanza kuwatafuta kwa kushirikiana na zimamoto tangu Machi 27, mwaka huu, tulipoanza mpaka sasa hakuna matumaini yoyote na sasa tunasitisha uokoaji," alisema.

Mkaguzi wa Mgodi huo, Fredy Ng'osha, alisema baada ya kupata taarifa kutoka kwa baadhi ya wachimbaji wadogo kuwa wenzao wamefukiwa ndani ya mashimo, walifungua njia nyingine ya kupita kuingilia katika mashimo hayo kutokana na njia iliyokuwa ikitumika awali kujaa maji lakini hawafanikiwa kukuta mtu ndani yake.

Alisema, wamekuwa wakifanya ukaguzi mara kwa mara kabla na baada ya kuingia mashimoni na yale yanayobainika kuwa na tatizo wachimbaji wake wanazuiwa kuingia ndani mpaka pale watakapofanya marekebisho na kukaguliwa upya, hivyo hawana uhakika kama mashimo hayo yatakuwa na wachimbaji ndani yake.

Mmoja wa wachimbaji, Samweli Jumbe, alisema taarifa hizo zilitolewa na baadhi ya wachimbaji lakini mpaka sasa hajapatikana mchimbaji hata mmoja katika mashimo hayo.



Wananchi wa Tarime, mkoani Mara, wakishiriki uwekaji wa alama za mpaka wa Hifadhi ya Taifa Serengeti (SENEPA), juzi. Alama hizo zinawekwa kwa mujibu wa sheria na makubaliano ya wananchi ili kutambua maeneo ya shughuli za kibinadamu na yaliyohifadhiwa ili kuondoa migogoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 2/- kudhibiti magonjwa ya milipuko

**Na Titus Mwombeki,** BUKOBA

SERIKALI mkoani Kagera imepokea Sh. bilioni mbili kutoka serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa vituo maalumu vya kukabiliana na kudhibiti magonjwa ya milipuko ambayo yamekuwa yakitokea mara kwa mara.

Hatua hiyo inatokana na kuwapo kwa magonjwa ya milipuko ambayo yamekuwa yakiripotiwa katika maeneo mbalimbali ya mkoa sambamba na juhudi za kudhibiti yanapotokea katika nchi jirani.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, alibainisha kupokea kwa fedha hizo katika kikao na watumishi wa serikali na wadau mbalimbali wa elimu mkoani hapa kilichofanyika juzi ofisini kwake. Alisema, serikali imetoa fedha hizo kwa lengo la kudhibiti kutokea kwa magonjwa hayo.

"Nitumie nafasi hii kumshukuru Rais Samia Suruhu Hassan kwa namna alivyotusaidia katika kupambana na ugonjwa wa Marburg. Mpaka sasa ametoa na kuidhinisha Sh. bilioni mbili kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo maalumu tengefu vya magojwa ya milipuko mkoani kwetu," alisema.

Aidha, Chalamila aliwataka wakurugenzi wote wa halmashauri za Bukoba, Misenyi, Karagwe na Muleba, kutenga haraka kila mmoja eneo lisilopungua ekari 10 karibu na barabara litakalotumika kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo.

Maeneo hayo, alisema yanatakiwa yasiwe umbali wa zaidi ya kilometa moja kutoka katika barabara kuu na kwamba kwenye fedha hizo, wameelekezwa pia kuanza kwa kutengeneza barabara za lami.

Baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri hizo, waliahidi kutekeleza agizo hilo kwa wakati ili kusaidia upatikanaji wa vituo hivyo vitakavyosaidia kudhibiti magonjwa ya milipuko.

"Naishukuru serikali kwa kutoa fedha hizi ambazo zitakuwa msaada kwa wananchi wetu na mikoa ya jirani. Kwa ujumla tutahakikisha tunaainisha maeneo hayo mapema ili hatua za ujenzi zianze mapema," alisema Waziri Kombo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi.

ama
ALHAMISI APRILI 13, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Mikoa sita Kanda ya Ziwa inavyoteseka utapiamlo, yabuni operesheni**



Ukurasa 13

Tabianchi inavyotenganisha mume na mke Ukerewe



Ukurasa 14

**Wataalamu Ubungo waenda mtaani kufunza kinga marburg, kipindupindu, Uviko 19**

WAZIRI UMMY NA ORODHA MANUFAA...

# Nchini kunaposimama Kituo Mafunzo ya Usalama Ulinzi Mimea ndani ya EA

**Na Yasmine Protace**

MARA zote, maabara ya kisayansi ni sehemu ya kufanyia utafiti. Hadi sasa kumekuwapo na tafiti za aina mbalimbali, lengo ni kujua ukubwa wake kupitia maabara hizo.

Hapo kuna aina mbalimbali za maabara kwa ajili ya kufanyika utafiti, ikipitia teknolojia za kisayansi nazo zikisaidia kuchunguza tatizo lililopo kwa binadamu au wanyama na kujua ukubwa wake, kutokana na kutumika nyenzo na mbinu mbalimbali za kiteknolojia.

Mara zote, pasipo kuwapo changamoto za mlipuko ya magonjwa inapotokea, ni ngumu kubaini chanzo cha tatizo, hasa pale sampuli tajwa zitapelekewa na kufanyiwa kazi, kisha kutoa majibu stahiki.

Waziri wa Afya nchini, Ummy Mwalimu, anasema serikali itaendelea kuboresha huduma za maabara zake nchini, kwa kuzingatia matakwa ya ulinzi na usalama kibaiolojia, ikihakikisha usalama wa watendaji kazi na mazingira kwa ujumla, katika namna inayofaaa.

Waziri Ummy anatamka hayo hivi karibuni, kwenye hafla ya kufungua Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii kwenye a Kituo cha Kikanda cha Afrika Mashariki cha Mafunzo ya Ulinzi na Usalama wa Vimelea .

Anasema, hadi sasa serikali iko katika hatua ya kuhakikisha usalama wa afya za Watanzania na wote waishio ndani ya mipaka ya nchi inabaki salama.





Baadhi ya wadau katika uzinduzi wa Kituo cha Maabara ya Afya ya Afrika Mashariki. **PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE**

"Wizara inatekeleza viwango vya kitaifa na kimataifa, kuhakikisha vimelea hatarishi vinavyotokana na hatua za upimaji na tafiti ndani ya maabara, havisambai katika jamii na kuleta madhara kama vile milipuko ya magonjwa," anasema.

Pia, anataja kuteuliwa kwa kituo hicho, kunadhihirisha jinsi maabara ya taifa inaendelea kuaminika duniani, ikiwa na uwezo wa kupima vimelea hatarishi, kwa kuwa vinaweza kutoka kwa wanyama kwenda kwenye mazingira na baadaye kuathiri afya ya binadamu.

"Utekelezaji wa afya ya ulinzi na usalama ni suala mtambuka, baina ya wizara mbalimbali nchini. Hivyo, tunahitaji kuwajengea uwezo wataalamu wetu, kupitia kituo hiki tutapata fursa ya wataalamu wetu wa Tanzania kupata mafunzo ya kimataifa kwa gharama nafuu, kwani mafunzo hayo yatakuwa yanafanyika hapa hapa nchini". anasema.



Waziri Ummy Mwalimu akizungumzia jambo,wakati wa uzinduzi wa kituo cha Maabara ya Afya ya Jamii, Dar es Salaam.

Anaongeza kwamba tangu kutangazwa kituo hicho, wamekwishapokea maombi kutoka Chuo Kikuu cha Musinde Murilo, cha nchini Kenya, kikiwaleta wanafunzi wanaochukua shahada ya ulinzi na usalama wa vimelea, kwa ajili ya elimu kwa vitendo, hali inayodhihirisha kwamba ni maabara inayoaminika na ina uwezo stahiki.

Hapo Waziri Ummy hafichi shukurani kwa wadau wa Afrika CDC, pamoja na wadau wa maendeleo kwa ushirikiano wenye tija na thamani kwa Watanzania, akiwataka wahusika waendelee kutimiza wajibu wao, ili sekta ya afya iimarike kwa kuwa huduma bora kwa wananchi.

Mwakilishi kutoka taasisi Afrika CDC, Dk. Talkmore Maruta, anaipongeza serikali ya sasa chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ikitoa taarifa zinazohusu ugonjwa mpya nchini wa Marburg.

Ahadi yake ni kwamba, asasi ya CDC itaendelea kushirikiana na serikali kuwajengea uwezo wataalamu wa afya nchini katika kujiandaa, kutambua na kukabiliana na magonjwa ya milipuko.

Tanzania ikiungana na nchi ya Afrika ya Kusini, ambayo imeteuliwa kuwa kituo cha mafunzo kwa nchi za Kusini mwa Afrika. Tanzania iliwasilisha maombi ya kuteuliwa kuwa kituo cha maombi, mnamo Septemba 2022 na Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii imepatiwa asilimia 100 ya haki hiyo.

AFYA

# Mikoa 6 Kanda ya Ziwa inavyoteseka utapiamlo, serikali yabuni operesheni

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UTAPIAMLO, kimsingi ni ugonjwa unaoathiri ukuaji wa mwili na akili ya mtoto, hasa pale anapokosa lishe bora au kula vyakula vilivyokosa virutubishi.

Takwimu zinaonyesha hadi sasa, idadi ya watoto wanaopata ugonjwa huo inakadiriwa kuwa asilimia 42 na mara nyingi, huwapata watoto wenye umri chini ya miaka 18 na wanawake walio katika umri wa uzazi.

Sababu inayochangia hali hiyo, kuwapo ni tatizo kwa wazazi kutokufuata ushauri wa wataalam wa afya, kama vile matumizi ya njia za uzazi wa mpango, kutokuzingatia lishe sahihi kwa watoto, ambayo ni makundi matano ya vyakula bora na watoto kulishwa vyakula vya aina moja.

Nchini katika Kanda ya Ziwa, ndiko kunakoongoza katika tatizo la utapiamlo na udumavu, licha ya kuwa eneo linalozalisha vyakula vingi.

Hata hivyo, mkoa wa Geita ndio unaotajwa kuongoza kuwa na watoto wenye utapiamlo kwa asilimia 38.6 ya watoto wote, na zinazofuatia na asilimia zake katika mabano ni Kagera (34.2), Simiyu (33.2), Mwanza (27.9), Shinyanga (27.5), pamoja na Mara (23.2). Hapo anawataka maofisa lishe waje kusimamia suala la kuongeza virutubishi katika vyakula shuleni, ili kuondoa hali hiyo.

Kukabili hali hiyo, Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Global Alliance for Improved Nutrition (GAIN) na kampuni ya Sanku, zimebuni mradi wa kuhamasisha ulaji vyakula vilivyoongezwa virutubishi shuleni, kupambana na utapiamlo shuleni.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga Mboni Mhita, wa kwanza, akiangalia kiroba cha unga kilichoongezewa virutubishi mbalimbali vya lishe, kinachozalishwa na Kampuni ya Sanku. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA**

### MENEJA MRADI

Archard Ngemela, ni meneja wa mradi huo unaotekelezwa katika mikoa sita ya Kanda ya Ziwa, anasema katika kila shule zinazotoa chakula kwa wanafunzi, zinapaswa kuhakikisha zinanunua unga uliongezewa virutubishi, kwa lengo la kupambana na tatizo hilo mashuleni na kuondokana na kula chakula cha aina moja.

Anasema, jumla ya wanafunzi 120,000 wanatarajia kunufaika na uwapo wa mradi huo katika shule za msingi 240 ndani ya mikoa ya Mwanza, Geita, Mara, Shinyanga, Kagera pamoja na Simiyu, ikiwa ni sawa na wastani wa shule hizo 40 kwa kila mkoa.

Aidha, Ngemela anasema ni mradi unaotekelezwa katika muda mwafaka, ambao serikali imetoa maagizo ya kila shule ya msingi iwe na chakula cha wanafunzi na hilo litafanyika kwa kushirikiana na wazalishaji 75 wa unga uliongezewa virutubishi.

> **"Ukosefu wa lishe bora, huwasababishia watoto kupata hali ya utapiamlo ambayo viashiria vyake ni udumavu, ukondefu na uzito mdogo au uliokithiri.**



Viongozi mbalimbali wa ngazi za mikoa sita ya Kanda ya Ziwa waliopo katika sekta za afya na elimu wakifuatilia elimu ya utapiamlo na udumavu wakati wa uzinduzi wa mradi wa uhamasishaji, ulaji wa vyakula vilivyoongezwa virutubishi shuleni.

Ngemela anazitaka kamati hizo za shule, kununua unga katika viwanda vinavyoongeza virutubishi. Anafafanua: "Lishe ni suala la msingi katika makuzi na malezi ya mtoto ndani ya siku 1000.

"Ukosefu wa lishe bora, huwasababishia watoto kupata hali ya utapiamlo ambayo viashiria vyake ni udumavu, ukondefu na uzito mdogo au uliokithiri. Pamoja na jitihada ambazo serikali inafanya na wadau wa maendeleo, bado tatizo la utapiamlo nchini ni kubwa."

Anaendelea:"Ubora wa chakula chenye lishe shuleni, kinahitajika ili kuwakinga wanafunzi wetu na tatizo la utapiamlo. Kamati za shule kwa kushirikiana na wazazi, mnatakiwa kununua unga ulioongezewa virutubishi kwa wazalishaji wanaongeza virutubishi na sio vinginevyo na maofisa wetu wa afya na lishe mnatakiwa kuwa na jukumu la ukaguzi wa vyakula shuleni wakati wote."

### TAMISEMI/SANKU

Kaimu Mkurugenzi wa Lishe Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mwita Waibe, anasema hadi sasa ni asilimia 47 ya watoto wadogo nchini wapo vizuri kiafya, huku idadi ya asilimia 53 wana changamoto ya utapiamlo na asilimia 30 wana udumavu na huko nyuma kwamba mwaka 2015/2016, jumla ya watoto milioni 2.9 walikuwa na udumavu mkubwa.

Anaeleza kwamba, kwenye mikoa hiyo, wanakabiliwa na changamoto ya utapiamlo na udumavu mkubwa na kinamama wenye umri wa kujifungua, wanaogoza kwa upungufu wa dawa, hasa kwa mabinti waliopevuka.

Hapo anasisitiza kwamba, lengo la serikali la kuleta mradi huo, ni kuhakikisha tunaongeza virutubishi na madini mengine katika vyakula vinavyozalishwa.

Mtaalamu wa Chakula na Lishe kutoka kampuni ya SANKU Josephine Kimario, anasema tayari wameanzisha mashine maalumu za kuongeza virutubishi katika vyakula lishe na sasa wameshatoa mashine 848 nchi nzima, kati ya hizo kuna mkoa wa Shinyanga zipo 48 na wilayani Kahama zipo tano, lengo ni kufanikisha mapambano na tatizo hilo.

Anasema, hadi sasa kila siku kuna wananchi milioni tano wanakula ugali ulioongezewa virutubishi na mashine hizo zina uwezo wa kutambua viwango vya lishe au virutubishi vilivyomo ndani ya unga. Hapa anawataka wamiliki wa viwanda vya kutengeneza vyakula, waongeze virutubishi kabla ya kupeleka sokoni.

### DC WA KAHAMA

Mboni Mhita, ni Mkuu wa Wilaya ya Kahama, anayesema, pale mjamzito anapopata lishe bora, anaondokana na kujifungua mtoto aliye njiti, wafu au mwenye mgongo wazi. Hapo anawataka kuepuka matumizi ya pombe, sigara na dawa za miti shamba kutibu minyoo, badala yake wafuate ushauri wa wataalamu.

Anasema, mkoa wa Geita unaongoza kuwa na watoto wenye utapiamlo kwa asilimia 38.6, ukifuatiwa na Kagera asilimia 34.2; Simiyu asilimia 33.2; Mwanza asilimia 27.9; Shinyanga asilimia 27.5; pamoja na mkoa wa Mara wenye asilimia 23.2.

Mkuu huyo wa Wilaya, anawataka maofisa lishe wa maeneo husika, kusimamia suala la kuongeza virutubishi katika vyakula kwa watoto waliopo shuleni.

Anataja mikakati inayofanyika sasa kwa ajili ya kupunguza utapiamlo huo katika mikoa hiyo, ni kwa kuendelea kuhamasisha wazazi kuhudhuria kliniki ya huduma ya mama, baba na mtoto kwa pamoja, ili wapate elimu ya malezi na makuzi bora ya mtoto, kunufaika na elimu ya lishe kwenye kliniki, hata kuendelea kutoa matone na vyakula dawa.

Mwingine ni kuwasisitiza kinamama kuwanyonyesha watoto, walio chini ya miezi sita maziwa ya mama pekee na kuwapa nyongeza ya chakula, baada ya miezi sita, ili kupunguza uwezekano wa watoto walio na umri chini ya miaka mitano, kuwa katika hatari ya kupata utapiamlo.

MAZINGIRA

# Tabianchi yatenganisha mume, mke

**Na Christina Mwakangale, aliyekuwa Ukerewe**



Wanawake wakulima wilayani Kakonko nchini Tanzania wakipokea mafunzo kuhusu mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. **PICHA: MTANDAO**

DEBORA Nyambuli (56), mama wa watoto saba, amekubali kubeba majukumu ya familia, baada ya mabadiliko ya tabianchi kubadili mfumo wa maisha yake na mumewe, kijijini Murutunguru, kitongoji Cha Namagamba, Wilaya ya Ukerewe, mkoani Mwanza.

Anasimulia namna maisha ya kisiwani humo yalivyobadilishwa na mabadiliko tabianchi na kusababisha kinamama kubeba majukumu ya kulea kaya.

"Mabadiliko ya tabianchi sio tu yametuathiri, yanaendelea kutuathiri. Mvua ni chache tofauti na zamani. Wanaume wenyewe wanaona ni ngumu, wengine wamehama."

Ukerewe ndani ya Ziwa Victoria, ni kati ya visiwa vidogo takribani 38, kati yake 20 vina makazi ya kudumu, vingine ya muda mfupi kwa ajili ya uvuvi.

Pia, ni kisiwa kikubwa ziwani ndani ya bara Afrika, pia cha pili duniani, kikiwa na eneo la kilomita za mraba 530 Kusini Mashariki mwa Ziwa Victoria, kwa mujibu wa Wikipedia, kilomita kadhaa kutoka jijini Mwanza.

**MAISHA HALISI**

Mkazi, mwanamama Debora, ni kati ya wanaoathiriwa na mabadiliko tabianchi, hata kuubadili mfumo wao wa awali wa maisha.

Anaiambia Nipashe hivi karibuni, kwamba: "Kilimo, uvuvi ilikuwa ndio shughuli kuu ya wanaume, lakini utakuta familia ina watoto saba, bado mke na yeye mwenyewe, anachokipata hakilingani na familia. Mwanaume anaona bora akae mbali asione kinachoikumba familia."

Anasema tangu Julai, 2021 mumewe alihamia mkoani Mara, akitelekeza familia na akitaja ni madhila.

"Wanaume wengine wamejaribu kuhamia huko huko kwenye uvuvi, nako samaki wanapata kidogo. Atafanyaje unafikiri? Anakaa huko huko. Sijui labda anaona anaumia kuleta nyumbani kitu ambacho hakitoshelezi," anaeleza Debora.

Anasema kalenda ya mvua na msimu wa kilimo umebadilika akisema: "Kwenye ekari moja na nusu nilipata gunia za mpunga 35, lakini sasa sioni dalili yeyote. Matarajio ilikuwa kuvuna Mei (2023), lakini sioni kupata kitu. Dalili za mvua utaziona kabisa ila inaweza isinyeshe, hata ikinyesha ni tofauti na zamani," anasema Debora.

Kwenye shamba hilo, Debora anasema amekwishawekeza shiligni 180,000 kwa ajili ya mbegu na mbolea, huku ikisalia miezi miwili kuvuna.

"Mwaka 2020 kilo moja ya mchele hapa Ukerewe, ilikuwa inauzwa Sh. 1,200 hadi 1,300 lakini sasa imefikia 3,000. Mahindi tunanunua kutoka kwingine, hatulimi hapa," anasema Debora.

Mwanamama mwingine mkazi wa kisiwa cha Kamasi, Ukerewe, Jasmine Deus, anasema sasa mlo wao ni maharage na dagaa, kwa kuwa samaki ambao zamani walipatikana kwa wingi, wameadimika.

"Ukila samaki sasa hivi unaonekana kama anasa. Dagaa ndio wapo, lakini bei ya juu. Kwa mtu wa kanda ya Ziwa kula maharage ni ngumu. Mkerewe hali maharage.

"Sasa hivi samaki sato mdogo shilingi 5,000. Nakumbuka nilipokuwa mdogo tulibadilisha bidhaa kwa kwa bidhaa 'butter trade' yaani ukiwa na unga wa ugali, unapewa dagaa, samaki," anasema Jasmine.

Juliana Mtabuzya, kutoka kata ya Bukindo, kutoka kikundi cha Songambele wanachama 15 kilicho na majukumu tofauti, anasema katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi aliamua kupanda miti ya michungwa 350.

Anasema pia, kuna michenza na milimao na mikakati yao kwenye eneo lao. kila mama awe amepanda miti takribani 10, kukabili hali hiyo.

"Tulikubaliana hakuna kukata miti ovyo, kwamba tusichome miti na misitu au mashamaba tutunze hali ya mazingira. Nililima ila sikupata zaidi," anasema Juliana.

Sixtaimelda Chilya, Katibu wa Kikundi cha Tunaweza, kinachofanya kazi kwenye kijiji Mibungo na Mabwewe, anasema umoja huo ulianza mwaka 2013 na kina wanachama 15.

"Kikundi kilipata mafunzo kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, tukaangalia tulime mazao gani kukabiliana na hali hii, tukaona tulime viazi vitamu na mihogo," anaeleza Sixtaimelda.

**WALIVYOFIKIWA**

Mkurugenzi wa Taasisi ya Sauti ya Wanawake Ukerewe, Sophia Donald anasema shughuli zao zimejikita wilayani Ilemela mkoani Mwanza, na kupitia ruzuku ya Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania (WFT-T), wametekeleza mradi uitwao 'Mwanamke Kabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi' kwa miezi mitatu, Agosti hadi Oktoba 2021.

Anataja visiwa vinne kati ya 20 vilivyopo eneo hilo; Bwiro, Bukungu, Irugwa na Kamasi na akitoa elimu inayowahusu wanawake. Anademas,wamefanikiwa kufika maeneo hayo, lakini visiwa vingine kuvifikia ni changamoto kutokana na jiografia na uhaba wa usafiri.

Sophia anasema taasisi inashirikiana na halmashauri kuandaa sheria ndogo, kumlinda mwanamke kwenye sekta ya mazingira, kukabiliana na mabadiliko hayo.

"Muhogo umepotea, njaa imeingia, wanaume wamehama Kwenda kutafuta shughuli nyingine za kufanya na kuachia familia zao huku wanawake wakitaabika na malezi.

Anasema kwenye mialo ya uvuvi, kunakuwapo kazi tofauti kwa wanawake, ikiwamo kuanika dagaa, pia kupata kazi ni ushindani mkubwa.

Sophia, anataja athari ya tatu waliyoibaini ni kupungua kwa samaki kwenye Ziwa Victoria, na kusababisha baadhi ya familia kukosa mlo, watoto wakipata utapiamlo.

Kupitia vikao vilivyoendeshwa na taasisi hiyo na kushirikisha wanawake, Sophia anasema mapendekezo yalikuwa ni kuwapo sheria ndogo, kumlinda mwanamke, msichana kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

> Ukila samaki sasa hivi inaonekana kama anasa. Dagaa ndio wapo, lakini bei ya juu. Kwa mtu wa kanda ya Ziwa kula maharage ni ngumu. Mkerewe hali maharage.

"Maadili pia yamepungua kwa sababu familia, baba, mama hawapo wameacha watoto wa kike ambao wengi wanapata mimba za utotoni.

"Utakuta wasichana wadogo wanafanya kazi kwenye migahawa, kwa ujira mdogo, hizo tayari ni ajira za utotoni," Sophia anasema.

Anasema ameshuhudia baada ya kufika Kata ya Umutungulu, walipokutana na wanawake wanane na kuhojiana nao, wanne walilalamikia waume zao wameachana, kwenda kuishi visiwa vingine.

"Ukerewe ina visiwa vinafikia 20 na vingine vidogo vidogo, Sasa pale wanapoishi hakuna Ziwa, inabidi waende kwenye visiwa vingine, hawezi kubeba familia yote. Wameona mvua haipo, ukame, wameona waende visiwa vingine. Kuna wakati wanaenda visiwa vya mbali, Sengerema, Bukoba," anasema Sophia.

"Tulikutana na mama mwenye umri kama wa miaka 36 ana watoto sita, ambaye ana watoto wadogo kimavazi walitakiwa kuwa nayo, hana, haja, hata huyo mama ni mjamzito ila ukimuona tu utabaini ni 'malnutrition'," anaeleza.

Sophia anasema athari za mabadiliko ya tabianchi, hayaonekana wazi, akifafanua:"Tunaambiwa shughuli za kibinadamu kukata miti zinachangia mabadiliko ya tabianchi. Lakini binadamu huyo akiona hapati alichokizoea, anatumia mbadala, kuna wanaovua kwa kutumia sumu ili apate samaki wengi kumbe ndio anaua mazalia. Na ndio maana saratani ipo zaidi huku Kanda ya Ziwa kutokana na uvuvi huo,"

"Rushwa ya ngono usipoiangalia vizuri inaweza usioanishe na mabadiliko ya tabianchi, ila tumebaini hilo, familia zimetengana kutokana na hali hiyo," anasema Sophia.

AFYA

# Wataalamu Ubungo waenda mtaani kufunza kinga marburg, kipindupindu, Uviko 19

**Na Beatrice Philemon**

HIVI sasa nchini kuna shida ya magonjwa ya kuambukiza mapya, ambayo ni Uviko 19 na marburg, pia kongwe la kipindupindu, ambayo yote kwa ujumla ni hatari kwa jamii.

Licha ya kuwapo hatua ya kitaifa inayochukuliwa na serikali kuikabili, pia katika ngazi ya kiserikali Manispaa ya Ubungo, kuna hatua inayochukuliwa ya tahadhari, badaa ya kutia shaka ya huenda ikaenea kwa wakazi wake kusiwapo mlipuko.

Hiyo inamaanisha kwamba, hata kukitokea hali hiyo kwa wenyeji, basi wawe kwenye ngazi ya tahadhari kwa kiasi fulani, ili kuweletea nafuu.

Katika hilo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, sasa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO), pia wadau wa afya wengineo, wameanza kuchukua hatua stahiki.

Ni hatua ya kujenga misingi ya tahadhari dhidi ya uvamizi wa maradhi kuelimisha wananchi, jinsi ya kujikinga na magongwa hayo.

## OFISA AFYA

Jamilah Nyoni, ni Ofisa Afya wa Manispaa ya Ubungo, anayesema hizo ni hatua za awali zinazochukuliwa, ili kujenga mazingira ya kijiamini dhidi ya kusambaa magonjwa hayo hatari, akiwataka wanachi wote kufanya mambo kadhaa.

Hapo anayataja kuwa ni kunawa mikono na maji tiririka na sabuni, mara baada ya kutoka chooni, kunywa maji safi na salama. Anaendelea: "Funika vyema tundu la choo baada ya kutumia.

"Epuka kusalimiana kwa kupeana mikono, epuka kula matunda yasiyooshwa kwa maji safi, epuka kula chakula mazingira yasiyo salama na epuka mikusanyiko isiyo ya lazima,"

Jamillah anasema, wameamua kuielimisha jamii ikiwamo ya wafanyabiashara na wanafunzi, kuhusu maradhi uviko -19, kipindupindu na kirusi cha Marburg, ili kama magonjwa haya yakitokea katika maeneo yao, tayari umama uwe na mwamko wa jinsi ya kujihadhari na kujikinga.

Anasema, hadi sasa wameashaanza kutoa elimu hiyo katika shule kadhaa anazozitaja kuwa ni Stendi ya Magufuli, Soko la Mburahati, shule za sekondari za Mbezi Inn na Kiluvya pia shule za Msingi Kiluvya.



Athuman Rajab, Mtoa Huduma Ngazi ya Jamii Manispaa ya Ubungo, akikabidhi 'sanitaiza' kwa Joshua Martine, mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Mbezi Inn, kwa niaba ya wanafunzi wenzake. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

## MTOA HUDUMA MANISPAA

Athuman Rajab, ni Mtoa Huduma Ngazi ya Jamii mkatika Manispaa ya Ubungo, anasema jumla ya wanafunzi 1812 katika shule za sekondari Mbezi Inn na Shule ya Msingi Mshikamano, wamepewa elimu jinsi ugonjwa wa uviko-19, kipundupindu na marburg unavyoambukizwa.

Katika hilo anasema kuna somo la kujua dalili zake, jinsi ya kujikinga, kitu wanachotakiwa kufanya mara wanapoona mwanafunzi au mtu anaumwa magonjwa hayo.

Anadems, ni elimu inayotolewa kupitia Mradi wa Mwaka mmoja unaojulikana kama 'Public Health and Social Resilience against COVID-19 and Other Communicable Diseases'.

Vilevile, UNIDO imeshatoa 'sanitaiza' na vipeperushi vinavyoelezea walimu na wanafunzi undani wa magonjwa hayo, yanavyoambukizwa, dalili zake, jinsi ya kujikinga nayo yakitokea, pia kufahamu namna ya kujikinga.

"Pia tuliwafundisha kuchukua hatua za haraka na kutoa taarifa kwa wataalamu wa afya au mwalimu wanapoona mgonjwa ili asiweze kueneza virusi kwa watu wengine, pia apelekwe hospitali mapema," anadems.

## DALILI ZA MARBURG

Kuhusu dalili za ugonjwa, mtu mwenye ugonjwa huo anakuwa na homa kali, akikosa hamu ya kula, uchovu, maumivu ya viungo, macho mekundu, kuharisha na kutapika damu, kuumwa tumbo, kupata vipele, kuumwa koo, pia kutoka damu puani.

Anasema wameamua kuwafundisha ili waweze kujikinga wenyewe na kuwakinga wenzao kwa sababu Uviko-19, kipundupindu na marburg ni magonjwa hatari nchini.

Inaelezwa kwamba, mwanamama anapokuwa na ugonjwa wa kirusi cha Marburg, anaweza kuambukiza mtoto wakati wa kunyonyesha. Anafafanua zaidi, akirejea jumuiyam ya wanafuzi akisema.

"Mwenzenu akipata hapa shuleni, anaweza kuwaambukiza, tuepuke kushikana na kupeana mikono hapa shuleni, pia mkiona mwanafunzi mwenzenu ana macho mekundu anataabika toa taarifa haraka kwa mwalimu ili apate msaada au apelekwe hospitali."

## SAUTI YA MWANAFUNZI

Joshua Martine, Mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari ya Mbezi Inn, anaishukuru UNIDO na Manispaa ya Ubungo, kutembelea shule yao na kutoa elimu ya Uviko-19, kipindupindu na kirusi cha marburg kwa wanafunzi.

"Tunaushukuru uongozi wa shule kuleta wageni hawa kwa sababu hatujawahi kupata elimu hii, mara nyingi tunasikia elimu hizi kupitia redio, au TV na si wanafunzi wote wanapata muda wa kusikiliza," anasema

Anafafanua kuwa, wanafunzi wengi wanaujua ugonjwa wa Uviko-19, hawajui kama kuna ugonjwa mpya, ni vema wataalamu wa afya walivyofika shuleni wametusaidia sisi, kupata elimu ya magonjwa hayo na kile cha kufanya.

"Sisi hatuna maji tiririka, tuna maji ya kisima ambayo tunatumia kumwagilia bustani, kusafisha vyoo, mimi namshauri mkuu wa shule atuwekee pia maji ya mabomba ambayo yatatoa maji safi yanayotiririka kwa ajili ya afya bora," anasema.

Pia, akaishukuru UNIDO kuwapa 'sanitaiza' wanafunzi, vipeperushi jinsi ya kujikinga na magonjwa haya.

Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Mshikamano, Rehema Missay, ana ufafanuzi akitamka: "ni kitu kizuri sana kwa elimu ambayo wametuletea."

## MWENYEKITI SOKO

Mwenyekiti wa Soko la Mburahati, Charles John anakubaliana na UNIDO, akiwa tamko " sisi kama wafanyabiashara tayari tumepata elimu jinsi ya kujikinga na ugonjwa wa korona na tulipewa vifaa vya maji tiririka, ili watu wakiingia sokoni wanawe."

Kwa mujibu wa mwenyeki huyo, ni vifaa vilivyotolewa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo, inayojumuisha tanki kubwa la maji na dawa ya kuweka kwenye maji na sabuni.

"Sisi kama wafanyabiashara bado tunahitaji elimu zaidi kuhusu magonjwa ya kuambukiza, hasa kirusi cha 'marburg', kwa sababu ndiyo inayotoa mwanga jinsi ya kujizuia au kujikinga," anaeleza na kufafanua Soko la Mburahati iliyoanzishwa mwaka 2019, kwa sasa ina jumla ya wafanyabiashara 160.

Maoni ya mwenyekiti huyo ni kwamba, utoaji elimu ya magonjwa ya namna hiyo, mara zote huishia kwenye ubora wa kujihadhari kiafya, hata kwenye ngazi ya familia.

> **Epuka kusalimiana kwa kupeana mikono, epuka kula matunda yasiyooshwa kwa maji safi, epuka kula chakula mazingira yasiyo salama na epuka mikusanyiko isiyo ya lazima.**



# Askofu awa mbogo ubadhirifu fedha

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Methodist Tanzania na Makamu wa Rais wa Kanisa hilo kwa nchi za Afrika, Joseph Bundala, ameishauri serikali kuwachukulia hatua wanaobainika kujihusisha na vitendo vya ufisadi ikiwamo kufilisiwa mali zao.

Aidha, amesema watakaobainika kujihusisha na masuala ya ushoga, usagaji, ndoa za jinsia moja na mauaji ya watoto, wanawake na watu wenye ulemavu wahukumiwe vifungo vya maisha jela.

Askofu Bundala alitoa rai hiyo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kukithiri kwa vitendo viovu vikiwamo vya ufisadi, ushoga, usagaji na ndoa za jinsia moja jambo ambalo ni chukizo mbele za Mungu.

Alisema akiwa nchini Benin, akizungumza kwenye mkutano mkuu wa kanisa hilo, alisema Tanzania haiungi mkono ufisadi, ushoga, usagaji, ulawiti ndoa za jinsia moja na ndoa za utotoni. Alisema licha ya sheria za Tanzania kutokubaliana na mambo hayo, mbele ya Mwenyezi Mungu bado ni chukizo.

"Nikiwa katika mkutano mkuu huo Afrika nchini Benin, nilikemea na kueleza kuwa ni laana na kwamba ni laana pekee itakayofanya Afrika ipigwe na Mungu japo umasikini unaokabili bara hili ni kama hautoshi hivyo Afrika tusikubali kupokea laana hiyo.

"Pia nashauri viongozi wa Afrika tusiogope kupinga na kukemea kwa nguvu kubwa vitendo hivyo vya ushoga na usagaji kwani Mungu atawapigania kwa kuwa kinachopigwa vita ni dhambi ambazo ni laana kwa kila mtu afanyaye kwani adhabu yake ni ziwa la moto," alisema.

Kuhusu ufisadi, alisema kwa mambo yanayoendelea nchini ya baadhi ya watu kujihusisha na matumizi mabaya ya fedha za serikali, kamwe lisifumbiwe macho na Rais anatakiwa kuchukua hatua za kisheria.

"Hivyo naiomba serikali ya Tanzania ione uwezekano wa kuwapo kwa sheria kali kwa mafisadi pamoja na watakaobainika wanajihusisha na ushoga, wafungwe kifungo cha maisha na kama ni mafisadi wafirisiwe mali na kuzirejesha fedha walizokula," alisisitiza.

# TBS yateketeza bidhaa za mil. 33.7/-

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) Kanda ya Kati limeteketeza bidhaa za chakula na vipodozi visivyo na ubora, zilizokamatwa kwenye maeneo ya bishara zenye thamani ya Sh. 33, 677, 6851.

Bidhaa hizo zilikamatwa kwenye maduka, maghala, baa, hoteli na Stoo katika halmashauri zote za Mikoa ya Dodoma, Singida na Tabora ambazo zinaunda Kanda ya Kati kwa TBS.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kuteketeza bidhaa hizo mwishoni mwa wiki, Ofisa Udhibiti Ubora wa TBS, Sileja Lushibika, alisema bidhaa zilizoteketezwa zimetokana na kaguzi zilizofanyika kwenye maeneo 41,44 kati ya Agosti, mwaka jana hadi Machi, mwaka huu na uzito wa kilo 3,509.09.

Lushibika alisema bidhaa za chakula zilizoteketezwa zilikuwa na uzito wa kilo 2,098.727 zikiwa na thamani ya Sh. 11,943,835 na vipodozi kilo 1,410.303 vyenye thamani ya Sh. 21,733,850.

Kwa mujibu wa Lushibika, bidhaa zilizoteketezwa ni zile zilizoisha muda wa matumizi, zenye viambato sumu na zile ambazo tarehe za mwisho wa matumizi zimeisha.

Alisema, madhara ya uwapo wa bidhaa ambazo muda wa matumizi umehariri wa na zile zenye viambatao sumu zinaathiri uchumi wa nchi pamoja na afya za watumiaji.

"Bidhaa za chakula zilizoisha muda wa matumizi na zile ambazo tarehe za mwisho wa matumizi zimehariwa zinaathiri upatikanaji wa virutubisho vinavyotegemewa, zinaweza kusababisha magonjwa ya muda mfupi na mrefu ikiwemo saratani," alisema.

"Kwa upande wa vipodozi hasa vile vyenye viambato sumu athari zake ni za muda mfupi, na mrefu ikiwemo kuathiri ngozi, macho, mfumo wa uzazi kwa akina mama, ukuaji kwa watoto na magonjwa ya saratani hasa ngozi," aliongeza.

Kwa mujibu wa TBS ukaguzi huo ni endelevu kwa mikoa yote na imetoa wito kwa wafanyabiashara kukagua bidhaa zao mara kwa mara kujiridhisha na ubora wake. Aidha, Lushibika amekumbusha wafanyabiashara kutunza bidhaa hizo kwa mujibu wa taratibu za wazalishaji, kuepuka kuuza bidhaa za vipodozi zenye viambato sumu na kutohariri taarifa za mwisho wa matumizi.

Aliwataka wazalishaji wa bidhaa kuthibitisha, kusajili bidhaa zao na wananchi wameshauria kutoa ushirikiano kwa shirika hilo endapo watakutana na bidhaa ambazo wanazitilia mashaka.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (katikati) akifurahia jambo na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto) pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela wakati wa futari iliyoandaliwa na benki hiyo katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma juzi. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Tume yabaini upungufu sheria uchaguzi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TUME ya Kurekebisha Sheria Tanzania imewasilisha ripoti mbili za mapitio ya sheria kwa Waziri wa Katiba na Sheria ikiwamo ya uchaguzi wa vyama vya siasa huku ikibaini kasoro tisa ikiwamo wanawake kunyimwa nafasi kulinganisha na wanaume.

Ripoti ya pili ni ya utoaji haki katika mahakama za mwanzo.

Akiwasilisha ripoti hizo Mwenyekiti wa Tume hiyo Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Januari Msofe, alisema utafiti umebaini kuwa kutokuwapo kwa sheria mahusus ya uchaguzi wa ngazi ya vijiji, mitaa na vitongoji, hivyo uchaguzi kuongozwa na kanuni zinazowekwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa (TAMISEMI).

"Aidha tume pia imebaini kujitokeza kwa uchache kwa wapigakura hali inayosababishwa na baadhi ya viongozi kutotekeleza ahadi wanazozitoa kwa wananchi wakati wa kampeni, hofu ya kutokea kwa vurugu eneo la kituo," alisema. Pia alisema, uwapo wa vituo vya kupigia kura mbali na makazi ya watu na kutokuwapo kwa sheria mahususi au mfumo unaowawezesha Watanzania walioko nje ya nchi na vizuizini kujiandikisha na kupiga kura.

Jaji Msofe alisema wadau wametoa maoni yao juu ya uandikishaji wa wapigakura njia ya kielektroniki kuwa hakuwezi kusimamisha demokrasia nchini, hivyo mfumo huo usitumike kwani nchi haijaendelea katika kuhakikisha usalama wa taarifa za uandikishaji na upigaji kura. Kadhalika, alisema wako wadau waliosema uchaguzi kwa njia ya kielektroniki uendelee kutumika kwa kuwa utaondoa udanganyifu na uboreshwe ili kuwapa nafasi watanzania wanaoishi nje ya nchi kushiriki upigaji kura, kuongeza ukweli na uwajibikaji katika upigaji kura.

Jaji Msofe pia alisema kutokana na wagombea kutakiwa kugharamia michango na matumizi yote wakati wa uchaguzi na sheria kukataza kupokea michango ya fedha au vifaa kutoka kwa wafadhili miezi mitatu kabla ya uchaguzi, wadau wameeleza kuwa sheria hiyo inawakandamiza.

Alisema utafiti umebaini uwapo wa sheria hiyo inawanyima fursa baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama hivyo kutoshiriki kikamilifi zoezi la uchaguzi kwa kushindwa kufanya kampeni.

Msofe alizungumzia pia mapitio ya mfumo wa sheria katika mahakama za mwanzo kwamba katika hilo wamekusanya maoni katika mikoa saba.

Alisema katika hilo utafiti umebaini kwamba mahakama hizo zilianzishwa kwa ajili ya kushughulikia mashauri ya mwanzo pekee na si mengineyo,na wadau wameshauri iondolewe sheria ya kuweka baraza la wazee.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alisema jukumu kubwa la Waziri wa Katiba na Sheria ni kupokea taarifa ya ripoti hiyo huku akiipongeza tume hiyo kutekeleza maelekezo yaliyotolewa Aprili, mwaka jana, wakati wakiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Dk. Ndumbaro alisema ilitolewa hoja juu ya ushiriki finyu na mazingira magumu ya wanawake kushiriki katika mchakato wa siasa,ambapo kwa mahusus kabisa sheria ya uchaguzi ilionyeshewa vidole. Alisema vyama vya siasa pia vilinyooshewa kidole ndipo wizara ikatoa maelekezo kwa tume kulifanyia kazi suala hilo.

Alisema Mwanasheria Mkuu wa serikali alitoa maelekezo ya kupitia taratibu za utoaji haki katika mahakama za mwanzo, hivyo leo amepokea taarifa za maeneo hayo.





# Mbaroni madai kuua mtoto wa kambo

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya, linamshikilia Zawadi Nzunje (30), mkazi wa Igalako wilaya ya Mbarali, kwa tuhuma za kumuua mtoto wake wa kambo, Meshack Mlawa (12), kwa kumpiga na kitu kizito kichwani kisha kukimbia kusikojulikana.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACP), Benjamin Kuzaga, jana alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Alisema Aprili 2, mwaka huu, mtuhumiwa alitoweka nyumbani kwake akiwa na mtoto huyo kwenda kusikojulikana na Aprili 4, ilifunguliwa kesi ya wizi wa mtoto katika kituo cha Polisi Igurusi.

Kutokana na tukio hilo, alisema walianza msako na Aprili 6 walimkamata mtuhumiwa na uchunguzi wa awali ulibaini kuwa chanzo cha tukio hili ni mgogoro kati ya mtuhumiwa na mke wake ambao ulisababisha chuki na hasira dhidi ya mtoto huyo, ndipo akapanga kumuua ili kumkoa aliyekuwa mke wake.

"Tulifanikiwa kumkamata mtuhumiwa akiwa eneo la Igurusi na alivalia kanzu na kuingia msikitini akijifanya na yeye ni muumini wa dini hiyo. Kwa taarifa za kiintejelensia weledi wa jeshi hilo, polisi walifanikiwa kumkamata," alisema.

Kutokana na tatizo hilo, Kamanda Kuzaga aliwashauri wanandoa kutatua migogoro yao kwa kushirikisha watu wa karibu, viongozi wa dini ili kupata suluhu ya mambo yanayowasibu.

Katika hatua nyingine, Jeshi hilo katika kipindi cha kuanzia Aprili Mosi hadi 11 lilifanya misako na doria kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa wa Mbeya na kuwakamata watu 44 kati yao wanaume 41 na wanawake watatu.

Miongoni mwa watuhumiwa hao ni waliohusika na mauaji, unyang'anyi wa kutumia silaha, kuvunja nyumba usiku na kuiba, utapeli, wizi wa mifugo na kupatikana na dawa za kulevya na pombe haramu ya gongo.

Alisema watuhumiwa wawili wanashikiliwa kwa tuhuma za kujihusisha na matukio ya unyang'anyi wa kutumia silaha eneo la Mlima Msangamwelu barabara ya Mbeya - Mkwajuni wilayani Chunya.

Kwa mujibu wa Kuzaga, watuhumiwa hao walitekeleza uhalifu huo Machi 23, saa 1:00 usiku. Wakiwa na wenzao wanne na silaha mbalimbali, waliweka magogo kwenye barabara na kuteka magari mawili yaliyotokea Mkwajuni kwenda Mamlaka ya Mji Mdogo Mbalizi yakiwa yamebeba bidhaa na wafanyabiashara.

"Watuhumiwa walipora fedha taslimu na vitu mbalimbali vya wafanyabiashara hao vikiwa na thamani ya Sh. milioni 11 zikiwamo simu za mkononi, mabegi na kisha kutoweka kusikojulikana na walianza upelelezi na kufanikiwa kukamata wawili," alisema Kuzaga.




Mkuu wa Idara ya Radiolojia wa hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Dk. Christina Mwagike akifafanua jambo kwa waandishi wa habari jijini humo jana, kuhusu kuanza kwa huduma ya mashine ya CT-Scan inayofanya kazi ya kupima magonjwa mbalimbali baada ya serikali kuinunua kwa gharama ya Sh. bilioni 1.5. Mashine hiyo, itaweza kuhudumia wagonjwa kati ya 70 hadi 100 kwa siku. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Ahueni kwa wagonjwa upatikanaji CT- Scan

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, imeanza kutoa huduma za CT- Scan ambayo ina uwezo wa kupima wagonjwa kati ya 70 hadi 100 wanaosumbuliwa na matatizo ya aina mbalimbali kwa siku.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Idara ya Radiolojia wa hospitali hiyo, Dk. Christina Mwagike, kifaa hicho ni cha kisasa na kina uwezo wa kupima magonjwa mbalimbali kwenye mwili wa binadamu na kutoa majibu kwa dakika tano hadi 10.

Akizungumza na Nipashe jana kwenye chumba cha kutolea huduma hiyo, Dk. Mwagike alisema tayari huduma hiyo imeanza kutolewa na kuwahimiza wananchi wenye matatizo mbalimbali kufika kwa ajili ya kupima afya zao na kufahamu magonjwa yanayowakabili. " Tunafurahi tunaanza kutoa huduma ya CT-Scan hospitalini hapa. Kulikuwa na uhitaji mkubwa wa kifaa hiki kwa sababu wagonjwa wengi walikuwa wanalazimika kwenda hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya au Muhimbili kupima. Lakini sasa tumepatiwa hapa na huduma zimeanza. Ni matumaini yetu wananchi kutoka maeneo mbalimbali watafika kupata huduma," alisema.

Dk. Mwagike alisema licha ya kupata kifaa hicho bado kuna uhaba wa wataalam wa mionzi hospitalini hapo. Kwa sasa kuna watumishi sita tu na uhitaji ni 13 ili kutimiza majukumu yao kwa weledi. Ofisa Habari na Mawasiliano wa Hospitali hiyo, Aggrey Mwaijande, alisema Sh. bilioni 1.5 zimenunua mashine hiyo ya kisasa yenye uwezo mkubwa wa kupima magonjwa mbalimbali ya binadamu.

Aliongeza kuwa lengo la ununuzi wa mashine hiyo ni kuboresha huduma za uchunguzi wa wagonjwa ambapo kitawasaidia madaktari kutambua uvimbe ndani ya mwili, matatizo ya moyo, magonjwa ya kichwa, miguu, wanaopata ajali na magonjwa yanayohusu viongo vya ndani.

Alisema uwapo wa mashine hiyo ni msaada mkubwa kwa wananchi kwa sababu itawapunguzia gharama kwa wagonjwa waliokuwa wanasafiri kuifuata mikoa mingine.

"Gharama za kupima kwenye mashine hii ni nafuu sana kwa sababu lengo la serikali ni kutoa huduma sio kupata faida hivyo mwananchi mwenye tatizo lolote asisite kufika hospitalini hapo kupata vipimo," alisema Mwaijande.

Isack Kyando, Mkazi wa Isyesye jijini Mbeya, aliishukuru serikali kuona umuhimu wa kununua mashine hiyo kwenye hospitali ya Rufani ya Mkoa na kwamba itasaidia kuokoa maisha ya wananchi na kuwapunguzia gharama za kuifuata huduma hiyo maeneo mengine.

Alisema awali huduma hiyo ilikuwa inapatikana kwenye hospitali binafsi na ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH) ambayo inaelemewa na idadi ya wagonjwa.

# Wananchi walia mfumuko wa bei

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAKAZI wa Jiji la Mbeya, wameiomba serikali kuingilia kati suala la mfumuko wa bei za vyakula na bidhaa nyingine kama mchele, mahindi na viazi mviringo.

Wamesema kwa sasa hali ya maisha imekuwa ngumu na bei ya bidhaa pia imepaa jambo ambalo limeibua malalamiko dhidi ya serikali kuona imeshindwa kudhibiti suala hilo.

Mmoja wa wakazi hao, Abdalah Muhidin, alisema mwanzoni mwa Machi, bei ya mahindi ilikuwa Sh. 20,000 kwa debe lenye ujazo wa kilo 20 lakini sasa bei imepanda mpaka Sh. 25,000 huku mchele ukipanda kutoka Sh 58,000 mpaka 60,000.

Alisema viazi mviringo vimependa kutoka Sh. 9,000 mpaka Sh. 12,000 kwa debe moja, hivyo aliiomba serikali kuingilia kati kudhibiti mfumuko wa bidhaa hususani katika kuelekea sikukuu ya Idd.

"Kwa kweli hali kwenye masoko ni mbaya kwani kwa mwaka jana miezi kama hii, bei ya mahindi tulikuwa tukinunua Sh 15,000 mpaka 17,000 huku mchele ukiwa Sh. 40,000 mpaka 45,000 na viazi Sh. 8,000 mpaka 9,000 kwa debe lenye ujazo wa kilo 20," alisema.

Mfanyabishara wa mahindi, Betwel Asumwisye, alisema huenda bei za mazao zikaendelea kupanda kutokana na hali ngumu ya uzalishaji wa mazao shambani kutokana na tatizo la upatikanaji wa mbolea.

Alisema tatizo lingine linalochangia bei ya bidhaa kupanda ni wakulima kuuza mahindi mabichi shambani na kusababisha upatikanaji wa mahindi makavu kuwa mgumu.

Mkulima kutoka kijiji cha Iwindi wilaya ya Mbeya, Anastazia Mwalwego, alisema hali hiyo imetokana na wakulima kutopanda mazao kwa wakati kutokana na uhaba wa mbolea pamoja na uhitaji mkubwa wa mahindi mabichi kwa wafanyabiashara wa Dar es Saalam na mikoa mingine.

"Mahindi mabichi yamekuwa na faida kubwa tofauti na yaliyokauka hivyo wakulima wanalazimika kuyauza yakiwa shambani ili kupata fedha zitakazowasaidia kukidhi mahitaji yao," alisema.



# Hemed aeleza azma serikali kuzalisha wataalamu wazawa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema serikali za Tanzania na Zanzibar zimejipanga katika kuzalisha wataalamu wazalendo watakaosaidia kuleta maendeleo.

Hemed aliyasema hayo jana katika uzinduzi wa kituo cha utafiti wa bahari, mazingira na maliasili uliofanyika viwanja vya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) Kampasi ya Betrasi mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema dhamira ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na Dk. Husein Ali Mwinyi ni kuhakikisha wataalamu wanapata ujuzi utakaotumika katika kuratibu na kushajihisha matumizi ya sayansi na teknolojia jambo ambalo litapelekea taifa kuwa na maendeleo ya haraka ya kijamii na kiuchumi.

Serikali ya Zanzibar, alisema imetilia mkazo sera ya uchumi wa bluu ili kuongeza pato la taifa na kuinua hali za wananchi kiuchumi na moja kati ya mihimili ya uchumi wa bluu ni uvuvi ambao unahusisha ufugaji wa mazao ya baharini.

Alisema uanzishwaji wa kituo cha utafiti wa bahari, mazingira na maliasili unaunga mkono juhudi za serikali na unaendana na azma na sera ya pamoja katika kuimarisha uchumi wa buluu.

Hemed pia alisisitiza kuwa kituo hicho ni vyema kifanye utafiti wenye tija kwa wananchi ili kutoa suluhisho la matatizo wanayokumbana nayo katika shughuli zao za ufugaji wa samaki.

Aliupongeza uongozi wa SUZA kwa kuanzisha kituo hicho hatua ambayo inatia moyo katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi Zanzibar kupitia sekta ya uchumi wa buluu.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Prof. Mohamed Makame Haji, aliishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa kuwaandalia miundombinu ya utafiti wenye mchango mkubwa wa kusimamia sera ya uchumi wa bluu.

Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, alisema mradi huo unatokana na ushindani uliohusisha taasisi za kitaaluma na kujumuisha maandiko 75 na andiko la Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.



Mwanamke anayefanya kazi ya uchongaji vyuma katika Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO), Flora Kwema (kushoto), akimfundisha kazi hiyo mwanafunzi wa mafunzo ya vitendo katika taasisi hiyo, jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Masauni akoleza vita vitendo ushoga, ukatili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, amewataka wazazi kutoa taarifa wanapobaini matukio ya mwenendo wa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia vikiwamo vya ushoga.

Amesema serikali imejipanga kuvidhibiti vitendo hivyo ili vijana wakue katika hali salama kwa maendeleo ya taifa.

Masauni alisema hayo jana alipozungumza na wananchi wa Jimbo la Kikwajuni katika hafla ya futari iliyofanyika katika ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul Wakil, mjini Unguja.

Alisema serikali haitakubali kuona vitendo vya matukio ya ushoga vinafanyika nchini kwa sababu ni kinyume cha maadili ya utamaduni wa wananchi wa Tanzania na Bara la Afrika.

Masauni alisema sheria za kudhibiti na kupambana na matukio hayo zipo na alilitaka Jeshi la Polisi kutumia sheria dhidi ya watu watakaobainika wanajishughulisha na mambo hayo.

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kamwe haitakubali kuwapo kwa matukio ya udhalilishaji wa kijinsia na vitendo vya ushoga ambavyo ni kinyume cha maadili ya utamaduni wa nchi yetu na bara letu kwa ujumla," alisema.

Aidha, Masauni aliwataka wananchi wa jimbo hilo kuongeza ushirikiano na umoja huku akizishughulikia changamoto mbalimbali zinazowakabili ikiwemo tatizo la maji safi na salama.

Akizungumza katika hafla hiyo, Katibu wa Jimbo, Khamis Rashid , alisema wanaunga mkono juhudi zinazochukuliwa na mbunge na mwakilishi wa jimbo hilo katika kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi wa jimbo hilo.

Baadhi ya wazazi waliohudhuria hafla hiyo, waliitaka serikali kupambana na vitendo vyenye unasaba wa ushoga ambavyo ni tishio kwa nguvu kazi ya vijana wa kiume.

Asha Haji Issa, mkazi wa Kikwajuni, alisema vitendo vya ushoga havikubaliki ambavyo ni sehemu ya uovu mkubwa na uchafu ambao unamkasirisha Mwenyezi Mungu.

# Wasisitiza kutumia haki uhuru kujieleza

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

OFISA Habari kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Zanzibar, Faki Mjaka, amewataka wananchi kuendelea kutumia vizuri haki ya uhuru wa kujieleza kwa mujibu wa katiba na kutoa maoni yao bila kumuumiza au kumdhuru mtu yeyote.

Akizungumza juzi katika warsha kwa waandishi wa habari na vijana kutoka asasi mbalimbali za kiraia na za kiserikali kuhusu uhuru wa kujieleza, alisema serikali zote mbili kupitia katiba zimetoa uhuru huo, hivyo si vyema kuvuka mipaka wakati wa kujieleza.

Faki alisema lazima kuheshimu serikali iliyopo madarakani pamoja na viongozi wake ili kutokwenda kinyume na uhuru huo.

"Kifungu cha 18 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 pamoja na ibara 19 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, wanachi wanapaswa kuutumia uhuru huo vizuri bila kuleta madhara kwa watu wengine," alisema.

Mjaka alisema katiba zote mbili zinapaswa kupongezwa kwa sababu zimetoa fursa kubwa ya uhuru wa kujieleza ambao unachochea uwajibikaji kwa viongozi.

Mratibu wa mradi wa BORESHA HABARI unaotekelezwa na taasisi ya Zanzibar Youth Forum chini ya ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Misaada la Marekani (USAID), Mussa Hija, aliwataka waandishi wa habari kutumia fursa waliyo nayo kutoa nafasi kwa wananchi mbalimbali kutumia vyombo vya habari kwa ajili ya kutoa maoni yanayohusu maendeleo ya nchi yao.

Alisema vyombo vya habari vya umma vinatakiwa kutumiwa na wananchi ili kutoa taarifa zao na matukio pamoja na changamoto zinazowakabili ili serikali ziwafikie na kuzifanyia kazi.

"Wananchi mnatakiwa mvitumie vizuri vyombo vya habari vya umma kwa ajili ya kuwasilisha taarifa zenu ikiwemo changamaoto zinazowakabili ili walengwa wazisikie na kuzifanyia kazi," alisema.

Baadhi ya washiriki wa mjadala huo waliitaka serikali kuifanyia marekebisho sheria ya habari ili kwenda na wakati wa mabadiliko yaliyopo ya kutoa habari kwa wananchi na kuondokana na vikwazo vilivyopo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ESTHER DANIEL SHAW anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya LANDROVER DISCOVERY 3 yenye usajili namba T539CKP, CHASSIS NAMBA: SALLAAA175A314886 na ENGINE NAMBA: ELD1119110019013. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: WMB/RB/63/2023

## KUPOTEA KWA CHETI



**ANAFI BARABARA SHEHE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0672-0145** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MKWAKWANI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MTN/RB/814/2022**

---

**FOMU MIRATH -2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**

**Kituo cha Moshi Mjini Kilimanjaro**

**Usimamizi wa mirathi Na 66 /2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU FATUMA RAMADHAN MLINGI WA MAJENGO KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUWA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SADIQ HAMISI ZULLU**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 24 Mwezi 04 Mwaka 2023 Kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo,3:00 Asubuhi
**Zingatia :**
Endapo kuna mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na wawea kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia
Imetolewa leo tarehe 3 Mwezi 04 Mwaka 2023

---

**IN THE COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No 35 of 2023**

**In the matter of the late MARIAM LUCAS CHILONGORA of MPAMAA within Dodoma region**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by JOEL MOSES KUYAVA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 17 day of 04/ 2023

Dated at Dodoma this 5 day of 04/ 2023

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTELEWA NA CHETI



**ROBERT B. BUNG'ERA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index number **S1625/0520** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **J.W. BUKANGA SEKONDARI** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MAR/MUG/RB/160731/2022.**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MBEYA**
**LILILOPO MBEYA**
**SHAURI No. 254/2018**
**ADAM MUSSA MBINDI..................MDAI**
**DHIDI YA**
1. **RAKI KAJETI LWESYA..................MDAIWA**
2. **AIZACK JOSEPH MLOTWA...............MDAIWA**
3. **SALEHE ALI............................MDAIWA**
4. **FINCA MICROFINANCE BANK.........MDAIWA**
5. **FRANET INVESTMENT COMPANY LTD**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA:**
**SALEHE ALI**
Fahamu kwamba ADAM MUSSA MBINDI amefungua Shauri dhidi yako katika Baraza hili.
Shauri limepangwa kwa ajili ya Hukumu tarehe 17/04/2023 saa 2.30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe Mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka usipohudhuria siku hiyo Baraza litatoa Amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 20/03/2023

**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**20/03/2023**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**DODEV ENTERPRISES CO.LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC.692 DKC** aina ya **SANLG.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.Taarifa ya polisi. **KAH/RB/251/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**KULWA ERASTO KAFULA** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne index No. S1176-0084 Mwaka 2019 Shule ya Sekondari BUSOLWA, kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**Taarifa polisi: KRU/RB/1385/2022.**

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA LILILOKO SONGEA**

**MAOMBI NAMBA 23/2023**

**DICKSON PIUS NDUNGURU ––––– MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **REHEMA KOMBA**
2. **ZAMDA MCHEKANAE ––––––WAJIBU MAOMBI**

**WITO /KUITWA SHAURINI**

Mjibu Maombi namba moja unataarifiwa kuwa Mwombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako.Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako,au wote kwa pamoja siku ya tarehe 17/04/2023 saa 2.00 asubuhi .Kumbuka pia nyaraka zote za kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zako za utetezi.

Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili upande mmoja bila kujali uwepo wako.

Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 03/04/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SAMWEL MOHAGACHI KEGOCHA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki **MC143DDV** SINORAY Iliyo tolewa na TRA. Taarifa imetolewa kituo cha polisi ARUSHA na kupewa kumbukumbu no. **ARU/ARU/RB/126653/2023.**

---

**FOMU MIRATHI - 2**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOROGORO VIJIJINI**

**Kituo cha MIKESE Mkoa MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi Na. 3 /2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU NASSORO RAMADHANI MTIBU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MGANGA NASSORO MTIBU**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11 Mwezi 05 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 3 Mwezi 04 Mwaka 2023.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WIMMO CONSTRUCTION** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **SCANIA** yenye usajili namba **T399CCZ.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kiuo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/127582/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA KILOSA**
**KITUO CHA RUAHA**
**MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA MADAI/NDOA Na 06/...2023**
**JINA LA MDAI: PATRICK BWANAFIKA NGUNWA**
**JINA LA MDAIWA: HALIMA KINDAMBA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:HALIMA KINDAMBA WA LIWALE**
**Kwa kuwa Mdai/Wadaiwa ameleta /wameleta madai yake/yao kwamba:TALAKA**
**NAMDAI MDAIWA TALAKA KWASABABU HATUNA MAELEWANO KWA MUDA MREFU PIA HATUPO PAMOJA KWA MIAKA SABA (7).**
Kwa hiyo unatakiwa Kuhuduria binafsi katika mahakama hii tarehe 03/05/2023 saa 02:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:**Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 05/04/2023

## KUPOTELEWA NA CHETI



**MICHAEL CELESTIN MUGANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S4213/0097** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MARIAN BOYS SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control Number: **9910836822219.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



ATHUMANI MUSSA MASANGULA anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba TAE208734 iliyotolewa uhamiaji makao makuu DAR ES SALAAM mnamo tarehe 01/10/2019. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: DAR/OST/RB/124539


# OFISI ZA MATANGAZO

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, Website: www.ippmedia.com**


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

## Nyaraka zilizovuja zaibua mapya vita Ukraine

**KYIV,** Ukraine

NYARAKA za siri zilizovuja mtandaoni zimeibua sura mpya dhidi ya vita ya Ukraine na Russia, baada ya kuelezwa kuwa moja ya faili hizo imebainisha kwamba Uingereza ni miongoni mwa nchi kadhaa zilizo na vikosi maalum vya kijeshi vinavyohudumu ndani ya Ukraine.

Siku chache zilizopita mitandao mbalimbali ya kimataifa iliripoti kuvuja kwa nyaraka za siri za Marekani, huku serikali ya nchi hiyo ikisema inachunguza chanzo cha uvujaji huo.

Inaelezwa kuwa nyaraka hizo zimethibitisha kile ambacho kimekuwa mada ya uvumi wa kimya kwa zaidi ya mwaka mmoja juu ya vikosi vya Uingereza kuhudumu Ukraine.

Inabainishwa kuwa faili zilizovuja, baadhi zikiwa na alama ya siri kuu, zinatoa picha ya kina ya vita vya Ukraine, ikiwa ni pamoja na maelezo nyeti ya maandalizi ya Ukraine ya kufanya mashambulio ya majira ya kuchipua.

Kwa mujibu wa waraka huo wa Machi 23 mwaka huu, Uingereza ina kikosi kikubwa zaidi cha vikosi maalum nchini Ukraine 50, ikifuatiwa na mataifa mengine ya Nato, Latvia 17, Ufaransa 15, Marekani 14 na Uholanzi kimoja, licha ya kwamba haielezi kuwa vikosi hivyo viko wapi au vinafanya nini.

Vile vile, inaelezwa kuwa idadi ya wanajeshi hao maalum inaweza kuwa ndogo, na kwamba uwepo wao nchini Ukraine huenda ukatumiwa na Russia, kwa malengo yake ya kuendeleza Propaganda kwani katika miezi ya hivi karibuni ilisema kuwa haikabiliani tu na Ukraine, bali Nato pia.

Kwa mujibu wa sera yake ya kawaida juu ya masuala kama hayo, Wizara ya Ulinzi ya Uingereza haijatoa maoni yoyote, lakini katika ujumbe wa Twitter uliochapishwa juzi ulisema uvujaji wa habari za siri umeonyesha kile ilichokiita kiwango kikubwa cha kutokuwa sahihi.

"Wasomaji wanapaswa kuwa waangalifu kuhusu kuamini madai ambayo yana uwezo wa kueneza habari potofu," ilisema.

Haikufafanua au kupendekeza ni hati gani mahususi ilikuwa inaizungumzia, huku maofisa wa Pentagon wakinukuliwa wakisema nyaraka hizo ni za kweli.

Hati moja, ambayo ilieleza kwa kina idadi ya waliopoteza maisha nchini Ukraine kwa pande zote mbili, ilionekana kuwa imefanyiwa ukarabati.

Pia inaelezwa kuwa vikosi maalum vya Uingereza vinaundwa na vitengo kadhaa vya kijeshi vya wasomi vilivyo na maeneo tofauti ya utaalamu, na vinachukuliwa kuwa kati ya vikosi vyenye uwezo zaidi ulimwenguni. **BBC**

# Upinzani Kenya waandaa mikutano ya hadhara


**NAIROBI,** Kenya

MUUNGANO wa vyama vya upinzani nchini Kenya umetangaza mipango yake kwa ajili ya mkutano wa hadhara, huku ukibainisha kuwa bado una dhamira ya kupunguza mvutano wa kisiasa kupitia mazungumzo, baada ya maandamano ya kuipinga serikali kugeuka ghasia.

**Muungano huo wa Azimio ulisema utafanya mkutano wa ndani ya ukumbi leo ukifuatiwa na mkutano wa hadhara unaotarajiwa kufanyika Aprili 23.**

Azimio la Umoja, Muungano unaoongozwa na mwanasiasa mkongwe wa upinzani, Raila Odinga, jana ulisema utafanya mazungumzo ya moja kwa moja na umma ikiwemo mkutano unaotarajiwa kufanyika mjini Nairobi, huku ukijiandaa kwa mazungumzo na serikali.

Aidha, mwezi uliopita kiongozi wa muungano huo Odinga aliitisha maandamano ya kuipinga serikali juu ya kushindwa kushusha gharama za maisha, na kwamba watu watatu walifariki, huku biashara na mali zikichomwa moto na kuporwa katika siku tatu za maandamano hayo.



Odinga (pichani), ambaye anadai aliibiwa uchaguzi wa rais wa mwaka uliopita, alisitisha maandamano baada ya Rais William Ruto kupendekeza wafanye mazungumzo kujadili hoja zao.

Muungano huo wa Azimio ulisema utafanya mkutano wa ndani ya ukumbi leo ukifuatiwa na mkutano wa hadhara unaotarajiwa kufanyika Aprili 23 mwaka huu ili kuwaelezea watu wapi walipo na hatua inayotarajiwa kufuatwa. **VOA**




Wakimbizi wa kiafrika wakiwa na mabango nje ya ofisi za Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) nchini Tunisia jana. **PICHA: DW**

# Waandamanaji waizingira ofisi ya UNHCR

**TUNIS,** Tunisia

WAANDAMANAJI wenye asili ya kiafrika wasio na makazi wameweka kambi nje ya ofisi ya Umoja wa Mataifa (UN) nchini Tunisia wakishinikiza kuhamishwa wakihofia baada ya utawala wa taifa hilo kuonyesha kutokuwa na imani nao.

Wahamiaji hao kutoka mataifa ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, waliweka kambi nje ya ofisi za Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) mjini Tunis kwa siku kadhaa, wakisema hawapo salama nchini humo, huku polisi wakitumia vitoa machozi kuwatawanya.

Mapema mwezi huu UNHCR ilitangaza inasitisha shughuli za uhifadhi duniani kote wakati ikihamia katika mfumo mpya wa usajili wa wakimbizi.

Famoussa Koita, raia wa Mali ambaye anatambuliwa na UN kama mdai halali wa hifadhi, alisema wamekuwa wakisubiri kwa takriban miaka miwili hadi mitatu kwa shirika hilo kukamilisha mchakato wake, na kwamba aliwaambia maofisa wa UNHCR watoke nje na kuzungumza na waandamanaji lakini ilikuwa tofauti.

"UNHCR walijaribu lakini watu hawakuwaelewa, kutokana na kile ninachokiona hapa chochote kinaweza kutokea wakati wowote," alisema.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani wa Tunisia Faker Bouzghaya, alisema polisi waliingilia kati kutokana na ombi la UNHCR na hadi sasa tayari waandamanaji takriban 80 wanazuiliwa na mamlaka.

Tangu Rais Saied alipodai bila ushahidi Februari kwamba wahamiaji kutoka Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara wanasababisha uhalifu na waliwakilisha njama ya mabadiliko ya kile alichokiita muundo wa idadi ya watu wa Tunisia ambao ni waarabu, wahamiaji hao wameendelea kusaka haki ya kuondolewa nchini humo.

Vile vile, inabainishwa kuwa muda mfupi baada ya hotuba ya kiongozi huyo, Waafrika weusi walikabiliwa na wimbi la ghasia na wengi wakiwemo wanawake wajawazito na watoto, ambao walifukuzwa kutoka kwenye nyumba zao na maeneo ya kazi na wamiliki wa nyumba na waajiri wakihofia kutozwa faini au kufungwa jela.

Jumuiya ya Kimataifa ililaani vikali matamshi ya Rais Saed kwa kile ilichokiita kuanzisha mashambulizi na wimbi la mitizamo ya chuki nchini humo. **DW**

# MINZIRO KICHEKO LIGI BARA, HITIMANA ALIA NA 'UZEMBE'

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

WAKATI benchi la ufundi la Geita Gold likiwapongeza wachezaji wake kwa kupata ushindi, Kocha Mkuu wa KMC FC, Thierry Hitimana, amesema bao la mapema walilofungwa lilichangia kuwavuruga katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyowakutanisha hapo juzi.

Kocha Mkuu wa Geita Gold, Fred Minziro, aliliambia gazeti hili siri ya ushindi wachezaji wake ni kutekeleza maagizo aliyowapa kuelekea mchezo huo ambao walipata ushindi wa mabao 2-0.

"Kabla ya mchezo nilizungumza na wachezaji wangu na kuwataka waingie uwanjani wakiwa na tahadhari, wacheze kwa kujihami, mbinu ambayo imewasaidia kupata matokeo mazuri tukiwa kwenye uwanja wa ugenini," alisema Minziro.

Alisema baada ya mechi hiyo, sasa wanakwenda kujipanga kwa ajili ya michezo iliyobaki kwa msimu huu na kuongeza malengo yao ni kumaliza katika nafasi za juu kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Kocha huyo alitaja siri ya mafanikio ya timu yake msimu huu imetokana na ushirikiano uliopo baina ya wachezaji, benchi la ufundi pamoja na viongozi.

Aliongeza pia aliamua kumchezesha, Kelvin Yondani, kama kiungo mkabaji baada ya Geofrey Manyasi, kuonyeshwa kadi nyekundu katika mechi ya robo fainali ya Kombe la FA Jumamosi iliyopita.



Hitimana alisema, amesikitiswa na matokeo waliyoyapata katika mchezo huo na kuwatupia lawama washambuliaji wake kwa kutokuwa makini katika dakika zote 90.

Kocha huyo alisema hawakutegemea kufungwa bao la mapema, halikuwa na kiufundi bali ni makosa ya kipa wake kwa kusimama vibaya huku akionyesha masikitiko yake kupoteza mechi hiyo.

"Nafikiri shida ni jinsi tulivyoanza, tulianza vibaya, tukaruhusu bao dakika ya pili tu na halikuingia kiufundi, baada ya hapo hawakucheza tena mpira wakawa wanalinda tu, ikatupatia kipindi kigumu sana kwa timu ambayo haishambulii," alisema kocha huyo.

Baada ya mechi hiyo, KMC imebakia katika nafasi ya 14 kwenye msimamo wa ligi hiyo wakati Geita Gold yenye pointi 37 imepaa hadi nafasi ya tano.



Wachezaji wa Geita Gold FC wakishangilia bao katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi. Geita Gold ilishinda mabao 2-0. **PICHA: TFF**

# *Shabiki MeridianBet ashinda nyumba*

**Na Saada Akida**

SHABIKI wa soka, Ernest Kisaka, mkazi wa Dar es Salaam amejishindia zawadi ya nyumba yenye thamani ya Sh. milioni 26 baada ya kubashiri kwa usahihi na Kampuni ya Meridianbet ya hapa nchini, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Meridianbet Tanzania, Martin Nkurlu, alisema ni kama ndoto iliyootwa usiku na mara ghafla imegeuka kweli kwa mshindi huyo ambaye aliyeweka mtaji wa dau la Sh. 20,000.

"Ushindi huu ni wa kawaida kuupata Meridianbet kwa sababu kila siku washindi wapya wanashinda katika kasino ya mtandaoni, unajiweka katika nafasi ya kushinda zaidi hata Mfalme huyu wa kubashiri soka alitengeneza mkeka wenye odds kubwa ya 1,439 na akashinda," alisema Nkurlu.

Aliongeza maisha ni rahisi kama utaichagua Meridianbet ambayo huwapa machaguo bora kila mechi, lakini bila kusahau kuna Jackpoti kubwa kabisa ya kushinda Sh. milioni 85 endapo utapatia ubashiri wa timu 13.

Naye Kisaka alisema tangu ameanza kubashiri na Meridianbet alikuwa anapata kiwango cha kawaida lakini jana ilikuwa ni bahati yake.

"Niliamua kuweka Sh 20,840/= na timu zangu 10, kila moja niliipa machaguo tofauti kwa kuwa Meridianbet wanatoa machaguo tofauti katika mechi moja," alisema Kisaka.

## Mbio za 'RUN FOR BINTI 2023' kufanyika Julai 2

**Na Frank Monyo**

SHIRIKA la Smile for Community (S4C) limeingia makubaliano na Shirika lisilo la kiserikali la Legal Services Facility (LSF)ya kuandaa mbio maalum za RUN FOR BINTI zitakazofanyika Julai 2, mwaka huu Dar es Salaam na baadaye Zanzibar ifikapo Desemba.

Mkurugenzi Mtendaji wa S4C, Flora Njelekela, alisema huu ni msimu wa tatu wa mbio za RUN FOR BINTI na mwaka huu wanatarajia zaidi ya washiriki 1,500 na kuweka wazi lengo la mbio hizo ni kukusanya rasilimali fedha kwa ajili ya kununua taulo za watoto wa kike.

Njelekea alisema shule za sekondari zitakazonufaika na taulo hizo pamoja na uboreshwaji wa miundombinu yake hasa katika maeneo ya vyoo zitakuwa za baadhi ya mikoa ya Mtwara na Lindi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, alisema moja ya malengo makuu ya taasisi yao ni kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wote hasa kwa wanawake na watoto wa kike.

"Tunaratibu mbio hizi kwa pamoja ili kukabiliana na changamoto ya watoto wa kike walioko shuleni kutopata haki ya kupata hedhi salama kwa sababu ya changamoto mbalimbali zinazowanyima fursa ya kukabiliana na hali hiyo pindi ikiwatokea," alisema Ng'wanakilala.

## Wanamuziki, wadau wamzika Hussein Jumbe

**Na Sabato Kasika**

WANAMUZIKI mbalimbali wa dansi, taarabu na bongo fleva walijitokeza katika mazishi ya mwimbaji mkongwe, Hussein Jumbe, aliyezikwa katika makaburi ya Kisutu jijini, Dar es Salaam juzi jioni.

Kiongozi wa bendi ya Sikinde Original, Abdallah Hemba, alisema wamepoteza jembe ambalo walikuwa wakilitegemea kwa sababu ya uzoefu wake katika kuimba na kutunga.

"Mwenzetu ametangulia imebaki zamu yetu tulio hai, hatujui ni lini, lakini kifo ni lazima, hivyo tujiandae, kwani wakati wowote, saa yoyote na siku yoyote tunaweza kukutana na umauti," alisema Hemba.

Alisema, alikuwa ameandaa mpango wa kushirikiana na Jumbe wa kuinyanyua bendi hiyo mpya, sasa umeishia hapo na kilichobaki ni kuendelea kumuenzi kwa kuendeleza mazuri yake yote.

"Binafsi ni mtundu wa kuiga sauti, hivyo nitaimba vipande vyote ambavyo alikuwa akiimba vikiwamo vya nyimbo zake kama nilivyokuwa nikifanya katika wimbo wa 'Nachechemea'," alisema.

## ZISIKUPITE

### GAVI ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA imefanya mazungumzo na wakala wa kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Hispania, Gavi mwenye umri wa miaka 18, kuhusu uhamisho wa bure kutoka Barcelona msimu huu. ***(AS)***

### MOUNT ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL imemfanya Mason Mount wa Chelsea mwenye umri wa miaka 24 kuwa kiungo wa kati anayelengwa msimu huu baada ya kujiondoa katika kinyang'anyiro cha kumsajili mchezaji mwenzake wa England, Jude Bellingham (19), kutoka Borussia Dortmund.***(Football London)***

### OSIMHEN AITAKA BAYERN

BAYERN Munich inafikiria kuwasilisha ombi la kumnunua mshambuliaji wa Napoli na Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen, 24, ambaye yuko tayari kuhamia klabu hiyo ya Bundesliga. ***(Sky Germany)***

### GALLARDO KUTUA CHELSEA

KOCHA wa zamani wa River Plate, Marcelo Gallardo, anawania nafasi ya ukocha wa kudumu katika klabu ya Chelsea. ***(UOL)***

### UNITED NA OFA MPYA

MCHAKATO wa zabuni ya kuinunua Manchester United unaingia katika raundi ya tatu huku wamiliki wa sasa (Glazers), wakishikilia kutaka ofa ya karibu ya pauni bilioni sita. ***(Mail)***

### BARNES AGOMBEWA ENGLAND

NEWCASTLE United ni miongoni mwa klabu kadhaa za Ligi Kuu England ambazo ziko tayari kumnunua winga wa Leicester City, Harvey Barnes, 25, ikiwa timu hiyo itashuka daraja. ***(Football Insider)***

### SHEA AGEUKA LULU

KIUNGO wa kati wa Manchester City na Ireland Kaskazini, Shea Charles, 19, analengwa na Leeds United, Brentford na Borussia Dortmund . ***(Guardian)***

### FIRMINO ATAJWA MADRID

REAL Madrid inafikiria kumsajili fowadi wa Brazil, Roberto Firmino, 31, kwa uhamisho wa bila malipo mkataba wake na utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. ***(El Nacional)***

### WEST HAM KUJIIMARISHA

KLABU ya West Ham inalenga kuwasajili Conor Gallagher, 23, kutoka Chelsea na Kalvin Phillips (27), wa Manchester City ili kuziba nafasi ya kiungo, Declan Rice (24). ***(Standard)***

### PRICE KUONDOKA EVERTON

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Ireland Kaskazini, Isaac Price, 19, anakaribia kufikia makubaliano na klabu ya Standard Liege baada ya kukataa mkataba mpya na Everton. ***(Liverpool Echo)***

### WOLVES KUMBAKISHA NEVES

KLABU ya Wolves inaandaa ofa mpya ya kwa kiungo wa kati wa Ureno, Ruben Neves, 26, ambaye hapo awali alikuwa akihusishwa na Arsenal na Manchester United. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# KIWANGO CHA SILVA CHAMPAGAWISHA PEP

**MANCHESTER,** England

Kocha huyo asema kiungo huyo ni mchezaji maalum, aonyesha makubwa wakiilaza...

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amemsifia kiungo, Bernardo Silva baada ya kiwango chake cha kuvutia katika ushindi dhidi ya Bayern Munich hapo juzi.

**Manchester City waliibuka na ushindi wa mabao 3-0 katika mechi ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na watapata faida nzuri kwenye mchezo ujao nchini Ujerumani katika mechi ya marudiano.**

Nyota wa Hispania, Rodri alifunga bao la kwanza kabla ya dakika 30, akipiga shuti kali la mguu wa kushoto lililojaa kwenye nyavu za kona ya juu.

Lakini lilikuwa ni bao la Silva ambalo lililoamsha furaha zaidi usiku huo - bao lake la kichwa likiwa la pili kwa City kabla ya Erling Haaland kuongeza la tatu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 alipewa nafasi ya kumshinda Riyad Mahrez, ambaye alianza katika mechi mbili zilizopita za Ligi Kuu England na michango yake ilikuwa ya kiwango cha juu zaidi kule Etihad.

Baada ya mchezo huo, kocha wake alishindwa kujizuia kumsifia kiungo huyo.

Alisema: "Ni mmoja wa wachezaji bora ambao nimewafundisha maishani mwangu. Yeye ni maalum.

"Bernardo Silva ni mchezaji wa mpira, inamaanisha nini? Atacheza kila mahali kwa sababu anaelewa mchezo. Bernardo ana uwezo wa kuusoma mchezo.

"Lakini Bernardo ni mchezaji muhimu sana katika aina hizi za michezo. Anaweza kucheza kiungo cha kati na hata namba tisa.

"Yeye ni mchezaji ukisema cheza katika nafasi hii, anaelewa kila kitu.

"Ulikuwa mchezo wa kuhitaji sana. Sasa inabidi nipumzike, siku ya mapumziko kwa vijana, kisha nijiandae kwa ajili ya Leicester.

"Nilijua kile tulichopaswa kufanya. Ikiwa hutafanya vizuri, Bayern wanaweza kufunga moja, mbili au tatu.

"Ni matokeo ya kushangaza, lakini lazima tucheze mchezo wetu tukiwa na tabia kubwa huko.

"Najua ushindi huu unamaanisha nini, lakini tunaenda huko kufunga mabao na kujaribu kushinda mchezo."

## HABARI MICHEZO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,102,0

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
SEVILLA
1 | 1.42
X | 4.25
2 | 7.00

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LIVERPOOL YAACHANA NA BELLINGHAM




**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imejiondoa katika mbio za kuwania kumsajili kiungo wa Borussia Dortmund, Jude Bellingham, msimu huu wa joto, huku klabu hiyo ikiamua kuweka fedha za uhamisho huo kwa ajili ya kukifanyia marekebisho kikosi hicho kinachonolewa na Kocha, Jurgen Klopp, vyanzo vimethibitisha ESPN.

Klabu hiyo ya Ligi Kuu England imekuwa ikihusishwa na tetesi za kumhitaji nyota huyo wa England kwa miezi kadhaa, lakini gharama ya uhamisho wake umeamua kujiweka pembeni.

Klopp ameweka wazi hitaji la kikosi chake kufufuliwa wakati wa msimu mgumu ambao unawafanya kudorora katika nafasi ya nane kwenye Ligi Kuu England. Huku kukiwa na mechi tisa za msimu huu, Liverpool wapo nyuma kwa pointi 12 kutoka nafasi nne za juu.

Kukosa kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya kunaweza kupunguza zaidi fedha zinazopatikana msimu huu wa joto na vile mvuto wao kwa walengwa wa kuhama.

Kocha wa Liverpool ameweka kipaumbele katika kuimarisha safu ya kiungo na wachezaji kadhaa wanaweza kuhitajika huku Alex Oxlade-Chamberlain, James Milner na Naby Keita wote wakiwa nje ya mkataba msimu huu wa joto.

Vyanzo viliiambia ESPN mwezi uliopita kwamba Manchester City walikuwa wanajiamini kwamba wanaweza kupata saini ya Bellingham, ingawa miamba wa Hispania, Real Madrid wanasalia kwenye mbio hizo.



# Lewandowski amtamani Messi

**BARCELONA,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Robert Lewandowski, amesema litakuwa "jambo la kufurahisha" kama Lionel Messi atarejea Camp Nou msimu ujao.

Mkataba wa Messi na Paris Saint-Germain unamalizika msimu huu wa joto, na vyanzo vimeambia ESPN kuwa hakuna uwezekano wa kusaini mkataba mpya.

Barca ilithibitisha kumekuwa na mawasiliano na nahodha huyo wa Argentina kuhusu uwezekano wa kurejea huku vyanzo vya ESPN vimesema anafikiria kuhamia Saudi Arabia kujiunga na Al Hilal, wapinzani wa jiji la Al Nassr ya Cristiano Ronaldo.

"Ikiwa atarejea Barcelona, itakuwa si kwa mashabiki tu bali kwa wachezaji kitu cha kufurahisha kwa sababu nafasi yake ni hapa Barcelona," alisema Lewandowski.

"Sijui nini kinaendel... ... natumaini msimu uja... tunaweza kucheza pam... ja kwa sababu najua kuw... Leo ndiye mtu anayewez... kufanya kitu bila ch... chote na bila shaka tun... hitaji aina hiyo ya wach... zaji, kwa hakika."

Messi anaweza kuo... geza mkataba wake... PSG huku kuhamia Li... Kuu ya soka ya Marek... ni uwezekano mwingine

## HABARI MICHEZO

82,037/-

# MANULA, KANOUTE, INONGA WAREJEA KUIKABILI YANGA

Na Adam Fungamwango

KIKOSI cha Simba kimeingia kambini jana saa 3:30 asubuhi kwa ajili ya kuanza maaandalizi ya mechi dhidi ya watani zao, Yanga itakayopigwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema wachezaji wote waliokuwa majeruhi wakiongozwa na Aishi Manula, Henock Inonga, Augustine Okra na Saido Kanoute wamerejea kikosini.

Ahmed alisema Kanoute hajaonekana kwa sababu benchi la ufundi liliamua kumpumzisha na si mgonjwa.

**“Kama utakumbuka katika mechi yetu ya robo fainali ya Kombe la FA dhidi ya Ihefu, beki wetu Inonga aliumia, alipata kidonda, ametibiwa na amerejea mazoezini na wenzake, Manula pia aliumia bega, akafanyiwa vipimo ikaonekana madhara yake si makubwa, akapewa mapumziko, naye amerejea mazoezini.**

Okra yeye alikuwa majeruhi muda mrefu, lakini alipona na ameshaanza mazoezi, hakwenda Mbarali kwa sababu hakuwa na utimamu wa mwili, lakini naye pia amerejea kambini,” alisema Ahmed.

Kuhusu kiungo mkabaji, Kanoute ambaye hajaonekana katika mechi tatu ni mzima na aliachwa kwa sababu ya kupata mapumziko.

Simba inahitaji kupata ushindi katika mechi hiyo ili kurejesha matumaini ya mbio za ubingwa wakati Yanga inataka kujiimarisha kwenye msimamo na hatimaye kutetea taji hilo wanaloliшikilia.



Kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), kilichoanza katika mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya wenyeji Algeria iliyochezwa juzi. Twiga Stars ililala mabao 3-0. **PICHA: TFF**

## Hatima ya Yanga, Fei Toto

INATOKA UK. 24

tofauti na hili, leo (jana), ambalo Fei Toto anadai kuvunja mkataba, kuchelewa kwa jambo hili ni kuhakikisha haki ipatikane kwa sababu kwenye haki hakuna haraka,” alisema Wambura.

Naye Wakili Fatma alisema hakuna chochote kilichoendelea zaidi ya kamati kuwapangia siku ya kusikiliza na kutoa uamuzi wa sakata la kiungo huyo.

“Mteja wangu (Fei Toto) ameshikilia msimamo hayuko tayari kurejea Yanga na anataka kuvunja mkataba. Kwa sababu kamati imetupangia siku nyingine basi mchezaji huyo ataendelea kufanya mazoezi yake ya kujiweka sawa akiwa nyumbani hadi hapo shauri litakapoamuriwa,” alisema wakili huyo.

Naye Simon alisema baada ya pande zote mbili kusikilizwa wamewasilisha pingamizi kwenye kamati hiyo na wamepangiwa tarehe husika.

“Yanga msimamo wake uko vilevile kama Fei Toto au klabu inayomhitaji kuvunja mkataba wanalazimika kufika mezani, tunasubiri hiyo siku ambayo kamati itatoa uamuzi wao,” alisema Simon.

## *Simba, Yanga*

INATOKA UKURASA 24

“Lazima wachezaji wetu watambue wanadhima kubwa ya kurudisha imani kwa mashabiki wa Simba kupata ushindi katika mchezo huu, kuna vitu vya kujivunia kwa sababu wachezaji wetu wako fiti, kuna watu wa kutuvusha salama ikiwemo Kocha Robertinho, lakini pia wachezaji wakijituma vizuri basi tutashinda huu mchezo,” alisema Ahmed.

Alimaliza ; “Itakuwa fedheha kubwa Yanga kutangaza ubingwa kwetu, itakuwa udhalilishaji Yanga kutangaza ubingwa, hatutakubali wapinzani wetu kutangaza ubingwa mgongoni kwetu. Hata kama tutakosa ubingwa basi hatutakuwa tayari kuwapa nafasi ya kutangazia ubingwa katika mechi yetu, hatuko tayari kuona wanatangaza ubingwa mgongoni kwetu,” alisema meneja huyo.


## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 15/04/23 | 17:00 | Wolverhampton Wanderers vs Brentford FC | 2.33 | 3.10 | 2.95 |
| 02. 15/04/23 | 17:00 | Chelsea FC vs Brighton & Hove Albion | 2.41 | 3.25 | 2.75 |
| 03. 15/04/23 | 17:00 | Southampton FC vs Crystal Palace | 2.60 | 3.10 | 2.60 |
| 04. 15/04/23 | 17:00 | Blackpool vs Wigan Athletic | 2.35 | 3.05 | 3.00 |
| 05. 15/04/23 | 17:00 | Queens Park Rangers vs Coventry City | 2.90 | 3.00 | 2.41 |
| 06. 15/04/23 | 17:00 | Stoke City vs West Bromwich Albion | 2.55 | 3.10 | 2.65 |
| 07. 15/04/23 | 17:00 | KAS Eupen vs SV Zulte Waregem | 2.33 | 3.40 | 2.75 |
| 08. 15/04/23 | 17:30 | Estoril Praia vs Portimonense SC | 2.38 | 3.00 | 3.00 |
| 09. 15/04/23 | 18:00 | Stade Rennes vs Stade Reims | 2.22 | 3.30 | 2.95 |
| 10. 15/04/23 | 19:15 | KV Oostende vs Oud-Heverlee Leuven | 2.48 | 3.45 | 2.50 |
| 11. 15/04/23 | 22:00 | Sparta Rotterdam vs SC Heerenveen | 2.23 | 3.30 | 2.95 |
| 12. 15/04/23 | 22:00 | America FC MG vs Fluminense FC RJ | 2.70 | 3.10 | 2.55 |
| 13. 16/04/23 | 00:30 | Botafogo FR RJ vs Sao Paulo FC SP | 2.49 | 3.05 | 2.80 |
| 14. 16/04/23 | 03:30 | Gimnasia Y Esgrima La Plata vs CA Belgrano | 2.30 | 2.75 | 2.90 |
| 15. 16/04/23 | 19:30 | Malaga CF vs FC Cartagena | 2.31 | 2.90 | 3.20 |
| 16. 16/04/23 | 20:00 | Union de Santa Fe vs CA Tigre | 2.60 | 2.85 | 2.47 |
| 17. 16/04/23 | 20:30 | VfL Wolfsburg vs Bayer Leverkusen | 2.75 | 3.35 | 2.32 |

## MECHI ZA USHINDI

“1” NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA “X” NI TIMU KUTOKA SARE “2” NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 13/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2802 | Eyupspor U19 vs Denizlispor U19 | 1.58 | 3.81 | 4.63 |
| 13:00 | 5751 | SC Farense U23 vs Rio Ave U23 | 2.03 | 3.01 | 3.63 |
| 13:45 | 3229 | PAOK Thessaloniki B vs FC Veria | 1.87 | 3.32 | 3.79 |
| 15:00 | 4039 | FC Samtredia vs FC Gagra | 2.26 | 3.06 | 3.01 |
| 15:00 | 4919 | Sioni Bolnisi-Dinamo vs 2 Tbilisi | 1.97 | 3.37 | 3.37 |
| 15:00 | 5104 | Hawassa Kenema SC vs Wolkite City FC | 2.15 | 3.01 | 3.32 |
| 15:15 | 2360 | TT Ha Noi vs Hai Phong | 1.60 | 3.54 | 4.93 |
| 15:15 | 5972 | Ho Chi Minh City vs SQC Binh Dinh | 3.90 | 3.49 | 1.76 |
| 15:30 | 1725 | Esperance Tunis vs Stade Tunisien | 1.42 | 3.65 | 7.61 |
| 16:00 | 1196 | QPR U23 vs Reading U21 | 2.18 | 3.90 | 2.60 |
| 16:00 | 2119 | Doxa Katokopia vs Olympiakos Nicosia | 2.09 | 3.32 | 3.32 |
| 16:00 | 2346 | Bandirmaspor U19 vs Samsunspor U19 | 2.97 | 3.74 | 1.98 |
| 16:00 | 4268 | EN Paralimni vs Nea Salamis | 2.34 | 3.23 | 2.91 |
| 16:00 | 4698 | Caykur Rizespor vs Sakaryaspor | 1.71 | 3.70 | 3.90 |
| 16:30 | 1794 | Rans Nusantara vs Persepam MU | 3.76 | 3.40 | 1.82 |
| 16:30 | 3727 | Persis Solo vs Persik Kediri | 2.34 | 3.24 | 2.68 |
| 17:00 | 2746 | Saburtalo Tbilisi vs FC Telavi | 1.60 | 3.64 | 4.99 |
| 17:00 | 4884 | PAOK vs Lamia | 1.20 | 5.41 | 12.49 |
| 17:00 | 5163 | Szentlorinc SE vs FC Gyori Eto | 3.14 | 3.09 | 2.14 |
| 18:00 | 5598 | Sidama Bunna SC vs Ethiopia Bunna SC | 3.10 | 2.89 | 2.32 |
| 18:05 | 1855 | Atletico San Luis U20 vs FC Juarez U20 | 2.16 | 3.33 | 2.87 |
| 19:00 | 3138 | Dila Gori vs FC Samgurali Tskaltubo | 1.83 | 3.27 | 4.05 |
| 19:00 | 5079 | Vejle BK vs Hvidovre IF | 1.86 | 3.44 | 3.55 |
| 19:00 | 5381 | MTK Budapest vs Haladas | 1.34 | 4.74 | 6.59 |
| 19:00 | 5999 | Budafoki Mte vs Diosgyori Vtk | 3.96 | 3.19 | 1.84 |
| 19:30 | 3441 | FC Tuerkiye vs Hamburger SV III | 2.07 | 4.09 | 2.69 |
| 19:45 | 1595 | Feyenoord vs Roma | 2.30 | 3.13 | 3.08 |
| 19:45 | 3071 | KAA Gent vs West Ham | 3.28 | 3.34 | 2.10 |
| 20:00 | 1179 | FC Otelul Galati vs Gloria Buzau | 2.20 | 2.93 | 3.19 |
| 20:00 | 2441 | El Fahem vs Hapoel Kfar Saba | 2.05 | 3.50 | 2.70 |
| 20:00 | 2510 | AS Ashdod vs SC Kfar Qasem | 4.85 | 3.27 | 1.76 |
| 20:00 | 3959 | Arsenal Sarandi vs Godoy Cruz | 2.91 | 2.86 | 2.46 |
| 20:30 | 4363 | Altay vs Altinordu | 2.27 | 3.30 | 2.73 |
| 21:00 | 4257 | Dibba Al Fujairah vs AL Wahda Scc (UAE) | 7.01 | 4.53 | 1.34 |
| 21:45 | 1139 | Dartford vs Taunton Town | 1.55 | 3.84 | 5.19 |
| 21:45 | 2306 | Al Arabi Doha SC vs Al Ahli Doha SC | 1.48 | 4.20 | 5.13 |
| 21:45 | 3090 | Concord Rangers vs Hungerford Town | 2.12 | 3.31 | 3.06 |
| 21:45 | 5069 | AL Wakrah vs Al-Shamal | 1.54 | 3.95 | 4.82 |
| 22:00 | 1347 | Anderlecht vs AZ Alkmaar | 2.59 | 3.10 | 2.69 |
| 22:00 | 1547 | Manchester Utd vs Sevilla FC | 1.42 | 4.25 | 7.00 |
| 22:00 | 2255 | Bayer Leverkusen vs Union Saint Gilloise | 1.56 | 4.04 | 5.26 |
| 22:00 | 4259 | Lech Poznan vs Fiorentina | 4.44 | 3.63 | 1.73 |
| 22:00 | 5587 | Juventus vs Sporting Lisbon | 1.88 | 3.22 | 4.20 |
| 22:00 | 5776 | FC Basel vs Nice | 3.42 | 3.27 | 2.07 |
| 22:15 | 3484 | Haras EL Hodood vs Zamalek | 4.41 | 3.01 | 1.90 |
| 22:15 | 5339 | Ismaily SC vs Enppi Club | 2.95 | 2.80 | 2.55 |
| 22:15 | 5619 | Arab Contractors vs Al Masry Club | 2.30 | 2.80 | 3.35 |
| 22:30 | 4312 | Colon Santa Fe vs Talleres | 3.15 | 2.99 | 2.23 |
| 23:30 | 4498 | Envigado FC vs Deportes Tolima | 2.81 | 2.97 | 2.46 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Alhamisi Aprili 13, 2023

Nipashe



Lewandowski amtamani Messi UKURASA 22

# Simba SC, Yanga mbio zimekolea

## ●●● Mnyama agoma kugeuzwa ngazi, Kaze afunguka wanajua hesabu za...

**Na Saada Akida**

BAADA ya ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Kagera Sugar, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema wameendelea kujiimarisha katika vita ya kutetea ubingwa wakati Simba imeweka wazi wataendelea kupambana mpaka filimbi ya mwisho wa msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2022/2023 itakapopigwa.

**Yanga yenye pointi 68 inaongoza katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali wakati Simba inafuatia ikiwa na pointi 60.**

Kaze alisema licha ya ushindi mnono waliopata, mechi hiyo ilikuwa ngumu kwa sababu walicheza kwa presha ya kusaka matokeo chanya ili kujiweka kwenye nafasi nzuri katika vita ya kutetea ubingwa wanaoushikilia.

Kocha huyo alisema kipindi cha kwanza cha mchezo huo kilikuwa kigumu zaidi na washambuliaji wake walikosa nafasi nyingi lakini waliendelea kupambana dakika 45 zilizofuatia na kufanikiwa kupata ushindi mnono.

Alieleza ushindi huo unawaweka katika mazingira mazuri na hali ya kujiamini zaidi kuelekea dabi ya Jumapili ambayo inatarajiwa kuwa ngumu zaidi.

"Tuna siku nne za kujiandaa kuelekea mchezo dhidi ya Simba, tumewaona wanavyocheza ubora wao, ni mechi ngumu kwa benchi la ufundi kwa sababu kila mtu anatakiwa kutia nguvu katika mchezo wetu huo wa dabi," alisema Kaze.

Aliongeza kupata ushindi katika mechi ya juzi kumewaongezea nguvu baadhi ya wachezaji ambao watataka kuendeleza kasi hiyo kwenye mechi inayofuata na hatimaye kutangaza ubingwa mapema.

"Matokeo ya dabi yatatuonyesha mbio za ubingwa, itakuwa na mechi nzuri na kila mmoja wetu anajiandaa vizuri kuelekea mchezo huo," alisema kocha huyo.

Pia Kaze alifurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na Stephen Aziz Ki ambaye alifunga hat-trick yake ya kwanza tangu atue nchini.

Naye Kocha Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda, amesema haiwi mwisho mpaka iwe mwisho, licha ya timu yao kupitwa pointi nane na vinara hao wa ligi.

Mgunda alisema bado wanaimani wanaweza kutwaa ubingwa wa ligi kwa sababu hadi sasa hakuna timu yenye uhakika wa kushinda taji hilo mpaka dakika ya mwisho.

Alisema ligi ni mbio ndefu na bado Simba iko katika mbio hizo na kueleza mechi ya mwisho ndio itatoa picha halisi ya vita hiyo ya watani wa jadi.

"Haiwi mwisho mpaka iwe mwisho, sasa nani atakuwa bingwa, anaongoza msimamo itajulikana mwishoni mwa msimu, sasa Simba tunapambana kuandaa timu kwa ajili ya kushinda mechi zetu zote zilizopo mbele yetu," alisema Mgunda.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema wameingia katika wiki ya watani wa jadi, wiki muhimu ambayo Wanasimba wanakwenda kufurahi.

"Sisi ndio wenyeji wa mchezo huo, tuna jukumu la moja kwa kwa moja kutangaza, jukumu ya kutangaza maandalizi ya mchezo na timu, kikosi kilirejea Dar es Salaam jana (juzi) na leo (jana), kinaingia kambini ili kuanza mazoezi maalum kuelekea mchezo huo," alisema Ahmed.

Aliongeza mechi hiyo ina thamani kubwa na wamejiandaa kupata heshima dhidi ya watani zao ambayo wameikosa tangu mwaka 2019.

INAENDELEA UKURASA 23



Mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki (kushoto), akijiandaa kumtoka beki wa Kagera Sugar, Abdallah Mfuko katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi usiku. Yanga ilipata ushindi wa mabao 5-0. **PICHA: MTANDAO**

# Hatima ya Yanga, Fei Toto Mei 4

**Na Saada Akida**

KAMATI ya Sheria na Hadhi za Wachezaji wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imepanga kutoa uamuzi wa mwisho wa shauri la kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto', la kutaka kuvunja mkataba na klabu ya Yanga ifikapo Mei 4, mwaka huu, imefahamika.

Kamati hiyo iliyoko chini ya Mwenyekiti, Said Soud, ilikutana Dar es Salaam jana ili kupitia mashauri mbalimbali ya wachezaji likiwamo shauri la nyota huyo ambaye Machi 6, mwaka huu alipeleka ombi la kuvunja mkataba na vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kamati ilitumia muda wa na dakika 55 kuwasikiliza Yanga na Fei Toto, ambapo Yanga walipeleka pingamizi la kutaka mchezaji huyo avunje mkataba kupitia klabu yao na si shirikisho.

Kikao hicho kilikuwa ni mapitio ya tatu baada ya awali TFF kuamuru Fei Toto ni mchezaji halali wa Yanga na anapaswa kurejea kikosini lakini upande wa mchezaji huyo haukukubaliana na uamuzi huo na kuomba marejeo.

Baada ya kuomba marejeo ya pande zote mbili, kamati iliamua nyota huyo bado ni mchezaji halali wa Yanga kwa mujibu wa mkataba wake ambao unamalizika ifikapo Mei 30, mwakani.

Fei Toto alifika TFF saa 5:31 asubuhi kwa gari aina ya Toyota Alphard yenye namba za usajili T569 DVC akiambatana na Wakili, Fatuma Karume 'Shangazi', Jasmin Razack pamoja na mama yake mzazi.

Yanga ndio walikuwa wa kwanza kufika katika ofisi za TFF, wakiingia kwenye eneo hilo saa 5:17 wakiongozwa na Ofisa Mtendaji Mkuu, Andre Mtine, Mkurugenzi wa Sheria wa klabu hiyo, Patrick Simon na wanasheria wengine.

Mkurugenzi wa Habari na Masoko TFF, Boniface Wambura, alisema kamati ilisikiliza pande zote mbili na kuzitaka pande hizo kurudi hapo Mei 4, mwaka huu ili kusomewa hukumu.

"Kamati itakutana tena Mei 4, mwaka huu kwa sababu shauri lililopelekwa kwenye kamati ni

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002